# SIMULIZI YAKE INAENDELEA.
# KITAMBAA CHA  PILI CHA SIMULIZI

# KITABU YA MATENDO YA MITUME.

# HUDUMA YA YESU KRISTO  KUPITIA YEYE BINAFSI NA MATENDO YA ROHO MTAKATIFU.

# KIONGOZI CHA MWALIMU.

KITAMBAA CHA SIMULIZI YA KITABU CHA MATENDO YA MITUME.

Utangulizi: Lengo la simulizi  ya kitambaa cha pili ni kuwasaidia wale wanafunzi (waumini) ambao wamempokea Yesu Kristo Kwamba wafundishwe simulizi ya kitambaa ili waweze kujua na kufikia ukombozi na mpango wa Mungu, Simulizi ya kitabu cha Mwanzo kupitia injili ya Yohana, Simulizi ya kitambaa cha pili imekita sana kwenye kitabu cha Matendo ya mitume na inaonyesha jinsi Yesu alivyotimiza ahadi zake kwa kumtuma msaidizi mwingine -  Roho mtakatifu, Baada ya kifo chake, kuzikwa na kufufuka (Tazama  YOHANA 14:16 – 18,26; 15:26-27; 16:7-15)

Nukuu: Lengo kuu la ujio wa Roho Mtakatifu ilikuwa ni kuja kuokoa na kuwaleta waliopotea watumike katika Nguvu ya Yesu Kristo, kila siku, nao waweze kuwafikia wote waliopotea, na kuwafundisha Neno la Mungu, na kufanya huduma kwa Jina la Yesu, Ni Nguvu ya Huduma ya Roho Mtakatifu pekee ndiyo inayomwezesha kila mwamini, katika kuishi na kujazwa Roho Mtakatifu, na kukamilisha kazi ya Mungu katika Mwili wa Kristo na Kanisa.

Hatua: kila picha imejumuisha simulizi ya Biblia, Maandiko yameambatanishwa kutokana na simulizi husika simulizi, Lakini usisome kwa wale ambao unashirikiana nao katika simulizi. Eleza Simulizi nyuma ya kila picha kama njia ya kubadilisha, na hapo mtu aanze kuifanyia kazi. Tumia Maarifa katika kumhekimisha kila mmoja katika kutengeneza kazi ya kila simulizi, katika maisha ya mtu mmoja mmoja. Kumbuka kutendea utamaduni au Desturi uliopo, Usitumie Utamaduni wa watu wa wengine tofauti na hao katika kushirikisha, Mfano watu wa utamaduni wa Magharibi hawawezi kuelewa katika yaliomo, Pia kumbuka kwamba tunaifadhi kila kitu tunachokifanya kiutamaduni ipatikananyo, wazawa na kustahimili binafsi (Hakikisha kwamba unaelewa Umuhimu wa Utamaduni wa watu unaojaribu kuwafikia)

Kazi: Eleza namna ya kuleta maarifa ya kufundisha kikamilifu ?

Swali: Jinsi gani ya kubuni kuwekeza kufundisha na kueleweshe.?

Nukuu: hakikisha kwa kurudia maandiko kulingana na simulizi kabla ya kushirikisha wengine, lakini kumbuka kwamba tunaelezea “simulizi” Jinsi Mungu alipofunua katika kitabu cha Matendo ya Mitume.

Mzunguko wa Ujumbe wa kitabu cha Matendo ya Mitume kuhusu mafunuo ya mtu na kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya waamini na kazi ya kanisa.

Kama unaonyesha picha ya Simulizi, shirikisha sehemu Muhimu za Maandiko kama vile unavyomweleza Mtu simulizi kuhusu kitu Muhimu.

Picha hizi zitatumika kukupa Ujuzi jinsi ya kufafanua simulizi

SIMULIZI SEHEMU YA 1: KUPAA KWA YESU. MATENDO 1:8 -11

Maandiko: Wale aliowadhihirishia Nafsi yake kwa dalili nyingi , baada ya kuteswa kwake, akafa na kufufuka, akawatokea Wanafunzi wake, akawa pamoja nao kwa muda wa siku arobaini , na kuyanena mambo yahusuyo Ufalme wa Mungu. Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu bali waingoje ahadi ya Baba , ambaye mliskia habari zake kwangu. (Matendo 1:3 -4) Yesu aliwaahidi tena wanafunzi wake .”Lakini mtapokea Nguvu akisha kuwajilia juu yenu Roho mtakatifu , Nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na katika uyahudi wote, na samaria na hata mwisho wa nchi, akiisha kusema hayo walipokuwa wakitazama ,akainuliwa , wingu likampokea kutoka machoni pao. (Matendo 1:8 -9 )

Kupaa kwa Yesu kinadhihirisha kwamba kusudi lake lilomleta Duniani Limemalizika, na hivyo alirudi mbinguni kwa Baba yake kwenda kusubiri mpaka ujio wake, mara ya pili utakapofika atarudi tena Duniani . hii huonyesha kuwa Yesu yuko Mbinguni akituombea kila mmoja wetu.

Simulizi: Yesu kabla ya kurudi kwa baba yake Juu Mbinguni , Aliwaagiza wanafunzi wake : Akawaambia “Basi Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi , mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu mkiwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi .(Mathayo 28:19 – 20a)

Yesu aliwapa ujasiri wa kutimiza Agizo hilo , kwa kuwaahidi Mambo matatu:

- Yesu aliwaahidi kwamba atakuwa pamoja nao kila mara: Nami nitakuwa pamoja nanyi hata ukamilifu wa Dahari. (Mathayo 28:20b)
- Na kwamba hatawaacha bila msaidizi: “Lakini huyo msaidizi huyo Roho Mtakatifu , Ambaye baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote na kuwakumbusha yote niliyowaambia .(Yohana 14:26)”
- Nao watapokea Nguvu baada ya kurudi kwa baba yake na ndipo Roho mtakatifu atakuja juu yao,: “Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu Yenu Roho mtakatifu, Nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem na katika uyahudi wote na samaria na hata mwisho wa Nchi. (Matendo 1:8)

Na kwamba wamsubiri Roho mtakatifu kuwajilia juu yao, ili waweze kuwa mashahidi, Nguvu ya Roho Mtakatifu itawasaidia wao kuwa mashahidi katika miji yote ya Yerusalemu na katika uyahudi wote na samaria Hata mwisho wa Nchi, {Matendo 1:8}

Samari : Yesu ametimiza unabii wote kama ilivyokuwa imetabiriwa kuhusu maisha yake ,kifo, ufufuo , Ametengeneza njia moja kwa wote wenye dhambi, ili waokolewe , Aliwaagiza wanafunzi wake na akawapa ujasiri wa kutangaza Habari njema ya wokovu ulimwenguni . Agizo kubwa ni uinjilisti na utume . na kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi na kuwafundisha kuyashika yale yote ambayo kristo aliwaamuru

Wajibu wetu: Kwa ujumbe wa malaika na Yesu kristo kupaa, Tunajifunza kwamba kusudi letu la kuishi hapa Duniani ni ili tuwe mashahidi wake na kuwahubiri injili na kuwafanya hata na hao tunaoishi nao kumpokea Yesu na hatimaye nao wawafundishe wengine wawe mitume kama wao.

Swali: Wapi Bwana amekuita wewe kuokoa na kutimiza agizo lake kubwa la kwenda ulimwenguni mwote kutangaza habari zake?

SIMULIZI SEHEMU YA 2: UJIO WA ROHO MTAKATIFU (Matendo 2)

Maandiko: Hata ilipotimia siku ya pentekoste walikuwako wote mahali pamoja, kukaja ghafla toka Mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliokuwa wameketi , kukawatokea ndimi, zilizogawanyikana , kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao, wote wakajazwa Roho mtakatifu, wakaanza kusema kwa Lugha nyingine kama Roho alivyowajalia kutamka . (Matendo 2:1 -4)

Simulizi: shirikisha jinsi gani mitume walikuwa pamoja , kuomba na kumsikiliza Mungu “Hawa wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja , katika kusali pamoja nao wanawake na mariamu mama yake Yesu na ndugu zake “( Matendo 1:14) na walipozidi kukaa pamoja kwa umoja , Roho mtakatifu akawashukia juu yao na akawajaza kwa nguvu na mara wakaanza kuhubiri injili kwa nguvu,Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja akapaza sauti yake akawaambia , Enyi watu wa uyahudi na ninyi nyote mkaao Yerusalemu , lijueni jambo hili mkasikilize maneno yangu. (Matendo 2:14.) Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya akisema, jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi, nao waliolipokea Neno lake wakabatizwa, na siku ile wakaongezeka watu wapata Elfu tatu,

Hivyo inawezekena kwa kila mmoja wenu . kama ukiomba na kumwamini Kristo , Roho mtakatifu sasa ataishi kwako na utaishi kama anavyotaka yeye.

Maisha ya kikristo huanza tu ukimruhusu Yesu Kristo kuingia ndani yako na kumwamini kama Bwana na Mwokozi wa maisha yako , na kila kitu kitawezekana, Alizaliwa na mwanamke bikira ,alifundisha katika huduma yake akiwa duniani,alikufa msalabani, alifufuka kutoka kwa wafu,kwa kufanya hivyo alionekana kuwa mtu mwenye Nguvu sana, yeye ni Bwana mfalme. Biblia inafundisha ukweli huu kwenye kitabu cha (warumi 14:9)” Maana kristo alikufa,akawa hai tena kwa sababu hii awamiliki waliokufa na walio hai pia.

Wajibu: Mungu amelipa kanisa Agizo moja tu ,kuwafanya wanafunzi. Hivyo kama umeokolewa ili uwe na uzima, Mungu amekuheshimu ili ushirikishe watu wengine unaoonana nao kwamba nini kimetokea kwako na utaona jinsi watakapompokea Yesu kristo kama Mwokozi , Na ni yeye peke yake ndiye anayeweza kusamehe Dhambi, kupitia kujitoa kwake kama Dhabihu ya Dhambi zetu.
Wale waliompokea yeye wataanza kuishi kama yeye anavyoishi na kwamba wamekwishaokolewa. Lakini hicho ni kitu ambacho hatuwezi kufanya sisi wenyewe, njia ni moja tu kuishi ndani ya Yesu kristo, na wokovu wake ni kupitia nguvu zake alizonazo , na chanzo chake inayotakiwa ni watu wote wajue na wawe naye: ni Roho Mtakatifu.
Swali: Mitume wana ukweli mkubwa na uzoefu wa kumjua Yesu, Lakini walikuwa wanahitaji vitu vingine vya ziada ili waweze kuwa na Amri kuu na kuishi maisha ya Imani katika Kristo, ambaye Yesu aliwawekea wafanye, Nguvu ya Roho Mtakatifu , kama umemwamini Yesu na kumpokea kama Bwana na mwokozi wa maisha yako, Roho Mtakatifu atatembea na wewe kwa mapenzi yake, kama utamruhusu kufanya kazi kwako, wewe mwenyewe utakuwa unapatikana binafsi?
Shirikishi: shirikisha ushuhuda wako umeokolewaje? Toa mifano ya kwamba kwa jinsi gani Mungu amekuwezesha na kukushirikisha wewe na kukuokoa wewe kwa Nguvu ya Roho wake?
Alafu waulize wasikilizaji wako wakushirikishe ushuhuda wao kwa sababu wanaweza wakawa hawajaelewa namna ya kutoa ushuhuda, Kuhusu Imani utamwelekeza na kumsaidia namna ya kusema “ ulikuwa unapenda nini kabla hujaokolewa , wakati Gani Yesu aliingia kwenye maisha yako , ni Tofauti gani umekutana nazo tangu uokolewe ? (Zote wokovu na mabadiliko ya maisha ni ujasiri wa Roho mtakatifu)

SIMULIZI SEHEMU YA 3 PETRO AMPONYA MTU KIWETE (Matendo 3:1-7)
Maandiko: Basi Petro na Yohana walikuwa wakikwea kwa pamoja kwenda Hekaluni ni saa ya kusali saa tisa na mtu mmoja aliyekuwa kiwete toka Tumboni mwa mamaye , alichukuliwa na watu ambao walimweka kila siku katika mlango wa Hekalu, uitwao Mzuri ili aombe sadaka kwa watu waingiao ndani ya Hekalu. (Matendo 3:1-2)
Baada ya Roho Mtakatifu kushuka juu ya Mitume, Walianzisha huduma yao na kueneza Habari Njema kumuhusu Yesu kristo, na namna ya kumpokea Yeye, Mungu alitenda miujiza Mingi Ili kuwaokoa watu wengi
Simulizi: waumini wa mwanzo walikuwa wakifuata Desturi za Dini zao kama walivyofundishwa na waalimu wao , kama ilivyo Desturi yao walikuwa wakienda kuomba na kuabudu kila siku , muda wa saa tisa mchana . Petro na Yohana walienda Hekaluni kumwabudu Mungu , ndipo wakamkuta mtu mmoja kiwete, mwenye miaka 40 , kiwete tokea kuzaliwa kwake (Matendo 4:22) Hawezi kufanya kazi, njia mojawapo aliyekuwa akijipatia msaada ni kuombaomba msaada.

Maandiko: “Lakini Petro akasema, mimi sina Fedha wala Dhahabu , Lakini nilichinacho ndicho nikupacho , kwa jina la Yesu kristo wa Nazareti Simama uende na akamshika mkono wake kuume akamwinua mara nyayo zake na vifundo vya vya miguu yake vikatiwa nguvu.“ (Matendo 3:6-7)
Simulizi : Petro alifahamu kwamba Mtu huyu alitakiwa alitakiwa amjue Mungu ili aweze kutembea , na hivyo akamwambia “kwa jina la Yesu christo wa Nazareti simama uende” na ndipo Yule mtu kiwete akaponywa sio tu kutembea, ameweza kuruka juu na kuinama na hapo akaanza kumtukuza Mungu, watu wakawa wanamshangaa kumwona yeye akiwa anatembea, kwa maana ukiwete wake ilikuwa tangu kuzaliwa kwake .

Hata miujiza ya kushangaza zilifanyika , kulikuwa kuna watu wengi waliokuwa wakiwaona mitume kama watu ambao walikuwa wakileta dini zao na kufanya zijulikane, (Matendo 4:4-5 )viongozi wa dini walikuwa wakidhihaki kulingana na Imani Zao na Desturi zao Hivyo hawakufurahishwa na ile injili ya kweli iliyowafanya watu wengi kuamini na kubadilika

Wajibu: Hizi miujiza ya nguvu ya Roho Mtakatifu ilikuwa ni kufanya Nguvu za Mungu kuokoa , pale ambapo Roho mtakatifu ametembea kwa nguvu, aliponya, ameokoa watu na kutenda miujza , kikubwa ilikuwa ni ukombozi kutokana na dhambi zetu. Pia ilikuwa kusudi ni Mungu atukuzwe na kuwawezesha watu wengine kutangaza, habari njema za ukombozi ambao wengine watamwamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wa Maisha yao.

Kumbuka wakati wa uwepo wa petro na mitume, Walishazoea kuwaokoa maelfu,nao walikuwa wakiwahudumia mtu mmojamoja, Roho Mtakatifu aliwapa Nguvu ya kuwahudumia watu wengi, Lakini Roho mtakatifu pia alimpa kila mtu Nguvu ya huduma kwa wakati wake.

Swali : kwa sababu alikuwa kiwete, Baadhi ya watu walimleta Yule kiwete mahali ambapo Mungu anaweza kumwokoa maisha yake. je? Ungependa uwe miongoni mwa wale wanaopatikana? Hata kama hujaelewa vizuri nini Mungu atende kwako? Nafasi ya huduma mara kwa mara huja isivyotarajiwa na watu, je utampa Mungu Nafasi ya kukutumia? je uko tayari muda wowote?

Nukuu: Yule mtu kiwete alimsifu Mungu , sio petro na yohana , aliyeponywa ndiye amechukua Nafasi ya kumwinua na kumsifu Yesu (Matendo 3:16) Ameponywa kama alivyokuwa anataka, alipokea kwa sababu ya kumwamini Yesu Kristo .

Muda wa ziada wa kufundisha: Chukua Muda kufundisha kuhusu Imani , ni sehemu mojawapo ya msingi katika Elimu ya mkristo ili kuelewa maandiko , kumbuka Imani hii imeletwa kupitia Kwa Yesu kristo , sio sisi (Waebrania 4:2) “maana ni kweli sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao , lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao , kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani ya waliosikia “kusikia maandiko tu haibadilishi maisha , ni kusikia na kuamini ndo inatakiwa , maandiko huambatana na Imani, Imani sio yale tunayoyauliza ili tupate Nguvu za Kiroho, Ni kile tu amabcho kinatuunganisha sisi na Yesu ,inayofanya kazi ndani yetu na anaishi kwetu kupitia Roho mtakatifu “ Yule mtu kiwete hakuponywa kwa sababu alikuwa na imani ya kutosha “ Aliponywa kwa sababu aliamini kwamba Yesu ni Nani, na nini Yesu anataka na Kile Yesu amesema alifanya , Katika maisha ya kikristo kiini cha iamni Yetu ni Yesu kristo , Ishara halisi kwamba sisi hatuwezi lakini yeye anaweza (Galatia 3:2) je mlipokea Roho kwa matendo ya sheria au kwa kusikia kutokana na Imani?)

SIMULIZI SEHEMU YA 4: YESU PEKEE NDIYE NJIA (Matendo 4:1-12)

(Onyesho kwa mtu aliyesimama pembezoni mwa njia)

Maandiko: “ Ndipo petro akijaa Roho mtakatifu , akawaambia enyi wakubwa wa watu na wakuu wa Israel” (Matendo 4:8) ‘Jueni ninyi nyote na watu wote wa Israel ya kuwa kwa jina la Yesu kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulubisha na Mungu akamfufua katika wafu kwa jina hilo mtu huyu anasimama alimzima mbele yenu (Matendo 4:10) “Wala hakuna wokovu katika mwingine awae yote kwa maana hakuna jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo “ (Matendo 4;12)

Simulizi: siku moja mitume wakawa wakiwaambia watu kuhusu ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu kwa sababu muda mrefu wamekuwa wakimsubiri Mesiya , Na vile walipokuwa wakiwaambia habari wale watu waliokuwa wakiwazunguka, Mkuu wa Hekalu, na Viongozi wengine , wakakasirika na kuwaadhibu na kuwajaribu ,Masadukayo walikuwa wakifanya hivyo kwa sababu walikuwa hawaamini ufufuo wa Yesu kutoka kwa wafu, walipowaweka katikati wakawauliza kwa Nguvu Gani na kwa Jina la Nani ninyi mmefanya haya ? (Matendo 4:7) Petro akajibu akawaambia " Ni kwa Jina la Yesu , Jina pekee chini ya Mbingu ambalo kwa hilo tunaokolewa" Muda wake alipokuwapo Duniani , Yesu alifundisha kuna njia mbili tu ambayo watu wanafata, Moja ni ya kukuongoza ukae mbali na Mungu na kujiamini na kujitumainisha Binafsi kwa vitu ambavyo ulimwengu wanafanya,- wanatoa , Njia Nyingine huongoza katika kuwa na Imani Binafsi katika ulimwengu na kumwamini Mungu.Ila kuna njia moja tu ambao watu wanaweza kuokolewa na kuja kwa Mungu ni kupitia Yesu kristo.

Hivyo Maisha mapya huanza ndani ya Yesu kristo , Unaweza ukafanya maamuzi je? Ni njia ipi utapita kwa ajili ya usalama wa maisha yako, kumfuata Yesu, au Mapenzi ya Mwili, Maisha binafsi, (ukiristo wa mwilini)

Wajibu : Kama utachagua njia ya kukuongoza kwenda kwa Mungu kupitia Yesu utaokolewa , lakini bado unatakiwa ufanye maamuzi mengine. Maamuzi ya kwamba utaendelea kutembea na Yesu kwa imani au kwa mambo unazoziona ulimwenguni.

Swali: kila Dhehebu lina taratibu zake : kwamba ni kwa jinsi gani kila mmoja wao wanamtafuta Mungu , wanatakiwa wafanyaje ili kumuhubiri yeye, na jinsi gani wamheshimu yeye? Kama ilivyo Nuru; Utamtafutaje Mungu mtakatifu? Utawezaje kumkaribia ?

Subiri jibu: Ni jambo Muhimu kwamba kila mmoja aliyempokea Yesu Kristo, amejua hii kweli Tangu mwanzo . waumini wapya wanatakiwa kujifunza na kuwa na mazoezi ya kwamba wanafahamu nini juu ya Mungu, Hakuna muujiza nyingine Paulo aliyoifanya kwa waumini isipokuwa kutembea na Yesu kwa jinsi hiyohiyo kama walivyo mpokea.

SIMULIZI SEHEMU YA 5: KUTOKUTII NI GHARAMA : Matendo 4:36-5:11.

Maandiko: Na Yusufu aliyeitwa na Mitume Barnaba, (maana yake Mwana wa Faraja) Mlawi asili yake ni Mtu wa Kipro , Alikuwa na shamba akaliuza akaleta Fedha akaweka miguuni pa mitume , Lakini mtu mmoja jina lake Anania pamoja na Safira ,mkewe aliuza mali , akazuia kwa siri sehemu ya Dhamani yake , Mkewe naye akijua haya akaleta Fungu Moja , akaliweka miguuni pa Mitume , Petro akasema Anania kwanini Shetani amekujaza Moyo wako kumwambia Uongo Roho Mtakatifu na kuzuia kwa siri sehemu ya dhamani ya kiwanja? Kilipokuwa kwako hakikuwa mali yako? Na kilipokuwa kimekwisha kuuzwa Dhamani yake haikuwa katika uwezo wako? Ilikuwaje hata ukaweka Neno hili Moyoni mwako? hukumwambia Uongo mwanadamu Bali Mungu , Anania aliposikia maneno hayo akaanguka akafa, Hofu nyingi ikawapata watu wote waliosikia haya. (Matendo 4:36 – 5:5)

Simulizi: (Eleza Simulizi ya Anania na safira kusisitiza Umuhimu wa kuishi maisha matakatifu yenye kujawa na ulinzi wa Mungu kila upande

Baada ya kuja kwa Roho Mtakatifu kanisa likaanza kukua na kushuhudia kwa wale watu waliokuwa karibu nao . Mwandishi wa kitabu cha Matendo ya Mitume Alielezea wawe na moyo mmoja na roho moja. (Matendo 4:32) walikuwa wanashirikiana kwa pamoja hasa hasa kwa wale wahitaji (Matendo 4:32 -35) (Kumbukumbu la Torati 15:4-11) Na mtu mmoja Jina lake aliitwa Josephu (Ambaye pia aliitwa Barnabas)

aliuza shamba lake na akaleta vyote alivyopokea kwa mitume ili zitumike katika shughuli zingine za kihuduma .
Mtu jina lake Anania aliona jose alichofanya na akaenda kuuza sehemu ya shamba lake na kupeleka sehemu ya pesa zake kwa mitume kama kawaida , Badala ya kumwambia Petro kwamba amejitengea baadhi ya hela kwa ajili yake mweneyewe, alidanganya na kusema nimeleta hela yote, petro aliongea na kusema! Anania kwanini shetani amekujaza Moyo wako na kumwambia uongo Roho mtakatifu. Na kuzuia kwa siri sehemu ya dhamani ya kiwanja ? (5:3).
Wewe hujafanya hivyo kwani – kwani si ilikuwa ya kwako wakati wote? Na Baada ya kuuza, kwani dhamani yote si ilikuwa ya kwako? Sasa ujue hukumwambia uongo mwanadamu bali Mungu" Basi petro alipomaliza kusema hayo , ndipo anania akaanguka hadi chini sakafuni Akafa, Na vijana wakaja wakamtia katika sanda wakamchukua nje wakamzika, na Hofu Nyingi ikawapata watu wote waliyoyasikia haya. Hata muda wa saa tatu Baadae mke wa anania, Safira akaingia ndani kuja kumwangalia na kumfata mume wake Hanania, Akiwa anaingia Ndani Petro akamuuliza! Akamwambia Niambie mlikiuza kiwanja kwa Dhamani hiyo? Naye akajibu Ndiyo kwa Dhmani hiyo, Petro akamwambia Imekuwaje hata mkapatana kumdanganya na kumjaribu Roho mtakatifu wa Bwana? Angalia miguu yao waliomzika mumeo ipo mlangoni nao watakuchukua nje wewe nawe, Mara akaanguka miguuni pake akafa ,wale vijana wakaingia wakamkuta amekufa, wakamchukua nje wakamzika pamoja na mumewe , hofu nyingi ikalipata kanisa lote na watu wote waliosikia haya." (Matendo 5:8 – 11)
Wajibu: Bwana anatutaka sisi tuwe wa kweli katika maisha yetu na hapo ndipo watu wengine watatuamini sisi, pale tunapowashirikisha ukweli wa Neno la Mungu kwao , shauku yetu ni kuwa na msukumo wa kuwaambia wengine kuhusu wokovu wa Yesu. Anania pamoja na Safira waliingiwa na kiburi , Zaburi 139: 23-24, Ni Andiko zuri la maombi ya kujichunguza kabla ya Mungu " Mungu Unichunguze na kuujua Moyo wangu ,unijaribu uyajue mawazo yangu, uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu ukaniongoze katika njia ya milele.
Swali: Fikiri juu ya matokeo ya hayo yaliyotokea kwa kila mmoja na yaliyoonekana , Jinsi gani ingekuumiza wewe kama ungekuwa hapo? Unafikiriaje juu ya Mungu kwamba anatufundisha nini kwa anania alivyodanganya?
Muda wa nyongeza wa Fundisho: kama Yesu alipowafundisha wanafunzi wake wokovu ilikuwa inaonekana kama vile wokovu ni bure lakini kumbe ina Gharama Yesu aliwafundisha, Yeyote ambaye hatabeba msalaba wake na kunifuata hawezi kwa Mwanafunzi wangu, Hakuna mtu awezae kutumikia mabwana wawili kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyu, ama atashikamana na huyu na kumchukia huyu, hamwezi kumtumikia Mungu na mali. (Mathayo 6:24)

SIMULIZI SEHEMU YA 6: GAMALIELI ASIMAMA MBELE YA VIONGOZI WA DINI
(Baraza la Yerusalemu) Matendo 5:27 -42
"Walioamini wakazidi kuongezeka waume kwa wake na hesabu yao ikaongezeka" (Matendo 5:14)
"Waumini wengi katika Bwana makundi ya wanaume na wanawake waliongezeka kwa idadi" matendo ya mitume 5;14
Maandiko: Walipowaleta wakawaweka katika baraza, kuhani mkuu akawauliza , akisema! Je hatukuwaamuru kwa nguvu msifundishe tena kwa jina hili? Nanyi tazameni mmeijaza Yerusalem mafundisho yenu na mnataka kuileta damu ya mtu Yule juu yetu , Petro na mitume wakawajibu wakisema, imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu, Mungu wa baba zetu amabye alimfufua Yesu ambaye Ninyi mlimwua mkimtundika katika mti , mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe mkuu na mwokozi awape waisraeli toba na msamaha wa Toba, na sisi tu mashahidi wa

Mambo haya pamoja na Roho mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wanaomtii, wao waliposikia wakachomwa mioyo wakafanya shauri kuwauwa. (Matendo 5:27-33)
Lakini mtu mmoja Farisayo jina lake Gamalieli mwalimu wa torati mwenye kuheshimiwa na watu wote, akasimama barazani akaamuru mitume wawekwe nje kitambo kidogo, akawaambia Enyi wanaume wa Israeli jihadharini sana jinsi mtakavyowatenda watu hawa .(Matendo 5:34-35)
“Basi nawaambia, jiepusheni na watu hawa , waacheni kwa kuwa shauri hili au kazi hii ikiwa imetoka kwa wanadamu Ina Mwisho, lakini ikiwa umetoka kwa Mungu hamwezi kuivunja, msije mkaonekana kuwa mnapingana na Mungu” (Matendo 5:8-39)
Neno la Mungu halizuiliwi, Mungu atatumia Neno lake milele kwa mtu Yule aliyemchagua yeye kufanya Neno lake lienee:

Simulizi: Wakati moja mitume wakifundisha Mkuu wa hekalu na Maafisa wake, Wakawaleta katikati ya baraza la makuhani , Wakisema hatukuwaamuru, ninyi kwa nguvu msifundishe tena kwa jina hili ? Ninyi tazameni mmeujaza Yerusalemu mafundisho yenu na mnataka kuileta damu ya mtu Yule juu yetu.” ( Matendo 5:28) Bali pamoja na kuongea kwao , petro alizidi kuongea kwa ukali
Petro na wale mitume wakajibu wakasema : imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu , Mungu wa baba zetu aliayemfufua Yesu ambaye nyie mlimuua na kumsulubisha msalabani, (Matendo 5::29-30) na sisi tu mashahidi wake, kwa jinsi gani tutaacha kumtangaza?
Petro alijawa na ukweli yeye na wengine walikuwa wakifundisha na kuishi kwa yale waliokuwa wakifundisha na iliwapa kuwa mashahidi wa Bwana Yesu hata kwenye sehemu za hatari kubwa.
Walisimama kwa ujasiri na kuwafanya wawe Imara zaidi Hivyo wakuu wa Dini Walitaka kuwauwa mitume, lakini Mfarisyo mmoja mwenye hekima jina lake Gamalieli akawashauri , Jiepusheni na watu hawa waacheni kwa kuwa kazi hii ikiwa imetoka kwa Binadamu Itavunjwa , Lakini ikiwa imetoka kwa Mungu Hamwezi kuivunja msije mkaonekana kuwa mnapingana na Mungu Wakakubali maneno yake , Nao walipowaita mitume wakawapiga kwa viboko na kuwaamuru wasifundishe tena kwa jina Hilo la Yesu, kisha wakawaacha waende zao ,
Nukuu Mwitikio wa wanafunzi, walitoka katika ile Baraza wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo, na kila siku ndani ya Hekalu na Nyumbani mwao hawakuacha kufundisha na kuhubiri , habari Njema za Yesu kwamba Ni Kristo. Matendo 5:41-42
Waliondoka kutoka kwa wakuu wa Dini wakaendelea kumuhubiri Yesu Wakijawa na Furaha , wakielewa mamlaka ambayo Yesu aliwapa, lakini hawakuogopa kupigwa kwa ajili ya kulifuata jina la Yesu.
Wajibu wetu: kumtii Mungu ni Bora zaidi kuliko kuwatii wanadamu , hata kama viongozi wa Nchi wanakulazimisha ufanye kitu ambacho Mungu hajakuagiza ufanye , au wakikukataza usifanye kitu ambacho Mungu amekuagiza ufanye inabidi ufanye tu.
Swali: Utataka kuwa chombo cha Mungu kutangaza Injili yake ulimwenguni, Hata kama kuna changamoto? Utakubali kwenda kwa Jina la Yesu?

SIMULIZI SEHEMU YA 7: STEFANO AHUBIRI MBELE YA VIONGOZI WA BARAZA- Matendo 7:1-53
Maandiko: Enyi wenye shingo ngumu msiotahiriwa mioyo wala masikio ,siku zote mnampinga Roho Mtaktifu , kama baba zenu walivyofanya na Ninyi ni vivyo hivyo , Ni yupi katika manabii ambaye baba zenu hawakumwuudhi? Nao waliwauwa wale waliotabiri habari zake Yule mwenye haki, ambae ninyi sasa mmekuwa wasaliti wake mkamwua, Ninyi mlioipokea Torati kwa Agizo la malaika msiishike, ( Matendo 7:51-53)
Muda mwingine kuna Gharama ya kulipa ili ulihubiri Neno.
Simulizi: Kuwasaidia viongozi katika kanisa la kwanza, wanaume saba walichaguliwa kuokoa, mmojawapo wa wanaume anaitwa Stefano, Aliyejawa na Imani na Nguvu za Roho Mtakatifu, Mungu

alifanya Ishara na maajabu kupitia Stefano. Na wengine walikubali na wengine walimkataa, walikutana pia na watu wengine wanaodanganya wakihubiri tofauti na kile Stefano anayoyahubiri, ambao waliwaweka watu katika mafundisho potofu, hivyo iliwaleta watu mbele ya Baraza la viongozi wa Dini, wakati kuhani mkuu alimuuliza Stefano kama kuna malipo ya lawama yaliyo ya kweli kuliko kujilinda binafsi, akapata Nafasi ya kuwakumbusha Historia ya wayahudi kwa jinsi gani tu wamemkataa Mungu ,Wakachagua njia zao binafsi za kuabudu nao wakamkataa Mwana wa Mungu ambaye ndiye Mesiya

Akahitimisha mazungumzo yake kwa kuwaita wao ,Enyi wenye shingo Ngumu msiotahiriwa mioyo wala masikio, (Matendo 7:51) Basi waliposikia maneno hayo wakachomwa mioyo na hapo wakaamua kumpiga na kumwua kwa mawe.

Wajibu wetu: Roho Mtakatifu atakupa ujasiri unapojisalimisha kwake na atakusaida wewe kuhubiri Injili pasipo woga wala sababu yeyote Katikati ya makundi mabaya , Stefano alitazama juu mbinguni akamwona Yesu akisimama upande wa kulia mwa Mungu, Na hii ilimpa yeye kutoogopa kabisa , waumini wa siku hizi hawana maono ya Yesu, Lakini tunaishi kwa Roho Mtakatifu ambaye tumepewa sisi kama nguvu hivyo ni lazima turudi kwake , Kumbuka kazi kubwa ya Roho mtakatifu katika muumini ni kumpa Nguvu katika huduma na Neno

Swali: Unadhani wewe ungechukua hatua gani, kama ungewekwa sehemu moja na Stefano? Imani yako ingeendelea? na ingebaki katika kumwamini Mung

SIMULIZI SEHEMU YA 8: KIFO CHA STEFANO – Matendo 7:54-60

(Stefano aliuliwa kwa mawe, na sauli amabaye baadae aliitwa Paulo alikuwa akishuhudia kifo cha Stefano.)

Maandiko: Basi waliposikia maneno hayo , wakachomwa mioyo wakamsagia meno , Lakini yeye akijaa Roho Mtakatifu akakazia macho yake, akitazama Mbinguni, akauona utukufu wa Mungu, Na Yesu akisimama upande wa mkono wa kuume wa Mungu, akasema Tazama naona Mbingu zimefunguka na mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume wa Mungu, wakapiga kelele kwa sauti kuu wakaziba masikio yao , wakamrukia kwa nia moja , wakamtoa nje ya mji wakampiga kwa mawe, nao mashahidi wakaweka nguo zake miguuni mwa kijana mmoja aitwae sauli , wakampiga kwa mawe, Stefano naye akiomba akisema , Bwana Yesu pokea Roho yangu, Akapiga magoti akalia kwa sauti kuu, Bwana usiwahesabie Dhambi hii,akiisha kusema haya akalala (Matendo 7:54-60)

Mungu alitumia tukio hili katika maisha ya Stefano na baadae kuleta mabadiliko kwa sauli, hakuwa na uwezo wa kuepuka lawama ambao Stefano alifanyiwa alipouwawa kwa mawe.

Simulizi: Viongozi wa Dini na watu wengine walimpinga Stefano, walijawa na hasira, na wote walimwinukia stephano, wakamchukua Nje ya mji nao wakaenda kumtupia mawe, nao wakamuuwa, wakachukua nguo zake wakaweka chini ya kijana mdogo aliembatana nao , nao wanamwamini na jina lake aliitwa Sauli, Nini ambacho Paulo angeona kuhusu maisha yake, Stefano akaangalia juu akamwona Yesu akisimama mkono wa kuume wa Mungu baba, akawaona watu wawili , na akamjua Yesu, hata hivyo Tukio ambalo linapaswa akumbuke ni Utawala Mungu na Nguvu za Yesu, yeye aliteseka kwa ajili ya jina la Yesu, watu wengi walianza kumpiga mawe, mawe yalipokuwa yanamlenga Stefano, akapiga magoti na kusema kwa sauti Bwana ,usiwalipize kisasi kwa dhambi hii bali uwasamehe na uwahurumie na hapo akafa. Hapo Stefano akawa mkononi mwa Mungu, na hakutendewa haki duniani lakini sasa Stefano anaendelea na Furaha na amani Mbinguni.

Wajibu wetu: Kitu cha kufanya katika maisha yetu ni kitu kimoja. Kumtukuza Mungu kwa kila kitu tufanyayo, wengine wanampokea yeye wengine hawamtaki, hata kama tukiishi au tufe, hili ni jambo

ambalo tumeliona kwake, wamemkataa stephano wanamkubali Musa na manabii wa Mungu, lakini kiukweli wanamkataa mwokozi wao Yesu kristo , Hapa ndipo penye ugumu na kuonekana kama sehemu maalumu ambao shutuma kubwa na dhihaka ya kanisa kuanza, Tukio ambalo lilihakikishwa kwa amri kwa uinjilisti , kulitumaini kanisa kwa maeneo yanayowazunguka.

Swali: Stefano amekuwaje mjasiri na mvumilivu wakati anaona kifo? Hii simulizi imekusaidia nini katika maisha yako? Wewe ni miongoni mwa wale waliompokea Yesu au wale waliomkataa Yesu? Na kama we ni Mfuasi uko tayari kweli kumfuata Yesu? Ingekuwaje kama ni wewe ndo unapitia kwenye mateso?

SIMULIZI SEHEMU YA 9: KANISA KIPINDI CHA MATESO – matendo 8:1-4

Maandiko: Na sauli alikuwa akiona vema kwa kuuwawa kwake Stefano,Siku ile kukatokea Adha kuu ya kanisa lililokuwa katika Yerusalemu , wote wakatawanyika katika nchi ya uyahudi na samaria ,isipokuwa hao mitume, watu watauwa wakamzika Stefano , wakamfanyia maombolezo makuu , sauli akaliharibu kanisa akiingia kila nyumba na kuwaburuta wanaume na wanawake na kuwatupa gerezani , lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri Neno. (Matendo 8:1-4)

Kanisa na waumini wote wako chini ya mateso lakini pamoja na hayo hesabu ya wakristo na watu wanaomwamini Yesu kama Bwana ilizidi kuongezeka zaidi

Simulizi: Kijana Mmoja jina lake Sauli, Aliyehusika na kumshuhudia Stefano akiuwawa kwa mawe, alikuwa akielewa zaidi kwamba wakristo wanafanya kitu ambacho siyo sahihi, kitu kibaya machoni pa Mungu, watu waliamini kwamba alihusika na kifo cha Stefano, kama ushuhuda wa kuweka zile mavazi miguuni pake, akajichagua mwenyewe kuwapiga waumini hata kuwauwa, yeyote atakayegundulika kama muumini, sauli mwenyewe aliendа nyumbani mwao na maaskari na kuwaweka wengine gerezani, yeye aligundulika zaidi akiwazuia watu wasiseme habari za Yesu, hivyo basi, mpaka utakapoomba Ruhusa kwenye eneo na kulipa kodi kwa vile wanavyotaka wao.

Nyongeza: wakati huu tunapata uwezo mkubwa wa kumtafakari Paulo baada ya maamuzi yake alipokuwa njiani akielekea Dameski (kwanini unaniudhi mimi?) pamoja na hayo alipata neema ,

Wajibu: Muda mwingi mateso huja kwa mtu pale atakapokuwa tayari kumfuata Yesu na kuwashirikisha na wengine , Hata hivyo walikuwa wakitenda haki , ingawa wamekuwa kama kwazo kwa wengine , nao kama watu waliochagua kushutumiwa watu wakapiga kelele kupinga hiyo huduma , ila kutokana na Maandiko tutahukumiwa endapo tutaacha imani hii yetu kwa miungu ya ulimwengu (Mathayo 5:10,12,
Yohana 15:20, 1Korinto 4:12)

Swali: Elewa kilichofanyika kama changamoto kama hayoYakikutokea utaendelea kumfuata Yesu ? Utaendelea kumtanagaza Yesu?

SIMULIZI SEHEMU YA 10: PETRO NA SIMON MCHAWI- MATENDO 8:18

Maandiko : Hata Simoni alipoona ya kuwa watu wanapokea Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume , akataka kuwapa fedha akisema , nipeni na mimi uwezo huu ili kila mtu nitakayemwekea mikono yangu apokee Roho mtakatifu, lakini petro akamwambia hela yako na ipotelee mbali pamoja nawe kwa kuwa unadhani ya kuwa karama ya Mungu inapatikana kwa mali, huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu, Basi Tubia uovu wako huu , ukamwombe Bwana ili kama yamkini usamehewe fikra hii ya moyo wako (Matendo 8:18-22)

Roho mtakatifu hanunuliwi , haongwi Yeye ni Zawadi kutoka kwa Mungu kwa kila mwamini atakayempokea Yesu Kristo kama Bwana na mwokozi wa Maisha Yake, sasa anakuja kukaa ndani ya

moyo wake, Wakati ukimpokea Yesu kristo kwa imani anakuja kwako milele na kukutia Nguvu katika Huduma ya ufalme wake , hivyo utalihubiri Neno la Mungu popote uendapo,

Simulizi: Simoni mchawi, mtu aliyekuwa akipunga mapepo na kufanya uchawi kwa Muda mrefu, alikuwa akiwafanya watu wa eneo lile, wamfikiri kwamba yeye ni Mtu mkubwa, alijionesha kuwa na nguvu kubwa na wengi walimwamini, kwamba alikuwa na Nguvu kutoka kwa Mungu ,hivyo wakatii kila alichokisema

Na wakati huo katika mji wao (mji wa Samaria) Mtume filipo alikuwa akihubiri na kutangaza habari za Yesu , na jinsi alipokuja kuokoa watu na Dhambi zao, watu wengi wakaamini mafundisho ya filipo, nao walioamini wakabatizwa vivyo hivyo simon naye akaamini, akabatizwa , akishangaa kwa ishara na miujiza ya filipo aliyoyafanya akapokea mabadiliko ya dhambi zake na kupokea toba yenye kuleta wokovu wa kweli.

Baada ya mitume huko jerusalemu kusikia kilichotokea huko samaria , petro na yohana wakaenda kuwafikia na kwenda kwa simoni na wengine waliokusudiwa kumpokea Roho mtakatifu

Ikawa siku moja mitume, wakiwaombea watu na kuwawekea mikono juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu ya wote walioamini ,

Simon akaja kwao . akauliza je? Ni kiasi gani cha pesa niwape ili na mimi niweze kupokea Roho mtakatifu, Petro akamwambia Rudisha hela yako , kwani zawadi ya Mungu hainunuliwi , na haiongwi kwani tumepewa kwa Neema , Hainunuliwi. Petro akamwambia huna fungu wala huna sehemu katika hili , kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu, Basi tubia uovu wako huu.

Wajibu wetu: Ni jambo la Muhimu na kujua kwamba pamoja na hayo simoni ameanza kuamini na kubatizwa kwa maji na kuombewa , Ila bado hakuwa mkristo (Kwani bado hajampokea Roho Mtakatifu – ukilinganisha Warumi 8:9) Wokovu wa kweli ni mabadiliko ya Moyo , kwamba usifuataishe matendo mabaya, mtu mwingine anaweza akajifanya.

Kumbuka Tafsiri ya Neno “Amini “ haimaanishi tu kuamini imani ( Ni mpaka uamini) Tazama (Yohana 2:23-25) (Yakobo 2:19) Imani ya kweli ni kwa Mungu pekee haijalishi ni kwa sehemu gani, lengo la simon alitaka nguvu ambaye atatumia yeye kwa manufaa yake kuliko kazi ya Mungu.

Swali : Utaamua kuwafundisha wengine ukweli wa kristo na kuwasaidia wakristo wengine kumwishia yeye na kukaa kwake kila siku?

SIMULIZI SEHEMU YA 11: FILIPO NA YULE TOWASHI – Matendo 8:26-39

Maandiko: “ Na walipokwisha kushuhudia na kulihubiri Neno la Bwana , wakarudi Yerusalemu wakahubiri Injili katika vijiji Vingi vya wasamaria, Malaika wa Bwana akasema na Filipo akamwambia, ondoka uende upande wa kusini hata Njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza nayo ni Jangwa , Naye akaondoka akaenda mara akamwona mtu wa kushi towashi mwenye mamlaka chini ya kandake, malkia wa kushi ,aliyewekwa juu ya hazina yake yote naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu, akawa akirejea ameketi garini mwake ,akisoma chuo cha Nabii isaya , Roho akamwambia Filipo , Sogea katika Gari hili ukashikamane nalo. Matendo 8:25-29.

Basi filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha Nabii Isaya akanena , Je yamekuelea hayo unayoyasoma? Akasema nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza? Akamsihi filipo apande na kuketi pamoja naye na Fungu la Maandiko alilokuwa akilisoma ni hili , Aliongozwa kwenda machinjioni kama kondoo , na kama vile mwanakondoo, alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya , vivyo yeye naye hafunui mdomo wake”.(Matendo 8:30-32)

“Yule towashi akamjibu Filipo akasema, Nakuomba nabii huyu asema maneno haya kwa habari ya nani ? ni habari zake mwenyewe au ni za mtu mwingine? , Filipo akifunua kinywa chake naye akianza kwa Andiko hilo hilo akamhubiri habari njema za Yesu. (Matendo 8:34-35)

Simulizi: Baada ya petro na Yohana kutoka samaria na kurudi nyumbani , Filipo akaanza kuwawaambia watu habari njema za Yesu, alipita katika vijiji vingi na kusafiri hadi kusini mwa Gaza, (Ambao ni 80 kilometers(mile 50) umbali . Siku moja malaika wa Bwana akamtokea yeye na kumwambia aende na apite barabara ya jangwa la kusini na akafanya hivyo , wakapita barabara ya vumbi ya Jangwani ambayo haikuwa nzuri kwa wasafiri

Wakati akisafiri mara akakutana na Mtu mkubwa ambaye alikuwa mtunza hazina kwa malikia wa Misri jina lake aliitwa Kandase . mtu alikuwa njiani akitoka kusherekea sikukuu ya wayahudi huko Yerusalemu, kama ilivyo desturi, kikatokea jambo la ajabu, Roho Mtakatifu alimwambia Filipo aenda na kusema na mtu yule, pamoja na hayo huyo mtu alikuwa ni mtu mkubwa wa serikali , Filipo alimkimbilia huyo mtu na kumwambia “ Nini hicho unachokisoma? Unayaelewa hayo? Yule mtu akamjibu, Nitaelewaje na sina mtu wa kunifundisha? Panda ingia garini mwangu na unifundishe , Mtu huyo alikuwa akisoma kuhusu unabii kuhusu ujio wa Yesu kama Masihi, Filipo akaanza kumfundisha na kumhubiria huyo mtu habari njema za Yesu, na hapo akaamini, yeye alijua kwamba njia mojawapo ya kumpata Mungu ni kupitia maandiko ya Agano la kale (Luka 24:45) Akaamini juu Ya Yesu kristo, na akamwomba filipo ambatize na Filipo akafanya hivo,. Pamoja na hayo watu wakawa wanamsikia Yesu kristo kupitia Filipo, Lakini Filipo akaonekana katika azoto na alipokuwa akipita akahubiri Injili katika miji yote hata akafika samaria.

Wajibu wetu: Roho Mtakatifu Atatuongoza sisi tuende kwa watu na kuwaandaa watu wampokee Yesu kristo , vyote tunavyotakiwa kufanya ni kumruhusu Roho mtakatifu atuongoze sisi.

Tunatakiwa pia kuangalia nje kwa wale wagonjwa , ambao wanahitaji mtu wa kuwaelekeza njia , wakimpokea Yesu kristo, bado wanamhitaji mtu wa kuwa makini nao na kuwafundisha na kuwaelewesha wao

Swali: Unadhani kwamba filipo alijipanga kumshuhudia Yule mtu? Kwamba achukue Muda na ajikusanyie nguvu, lakini tunayo agizo la kuwafundisha watu wengine habari za Yesu Wakati wowote uliokusudiwa na Mungu, Utakuwa miongoni mwa hao? (Nipe jibu)

Filipo amesafiri na kufikisha Habari njema kwa kila mtu aliyemwona , hata huko Gaza ambao ni miongoni mwa miji ya phalestina , Wakaona ni muhimu wao wawepo pale , wakati huo ilikuwa kama mtego lakini ona matokeo ya injili huko Ethopia , lengo haikuwa Misri Ethopia lakini cha kushangaza watu wameitikia injili yao.

Nukuu: Hii ni wakati wa kujifunza umuhimu wa ubatizo na maana yake, na kwamba mkristo mpya anatakiwa abatizwe, filipo alielewa kwa undani jambo hili, (Matendo 8:12) Tumia Warumi 6:1-10 kuelezea kifo, kuzikwa , ufufuo wa mtu aliyemwamini Yesu na kwamba ubatizo ni picha ya hayo kwamba ni Kifo, kuzikwa, ufufuo katika Kristo, Neno kubatiza (Batiza) humaanisha kuzamisha, Taz (Matendo 8:38) Ni kuzamishwa ndani ya maji , na (kupanda juu kutoka kwenye maji)

SIMULIZI SEHEMU YA 12: KUTOKEWA NA KUBADILISHWA KWA SAULI

Matendo 9:1-6,10-19

Maandiko: Lakini Sauli akizidi kutisha na kuwaza kuwauwa wanafunzi wa Bwana , akamwendea kuhani mkuu, akataka ampe Barua za kwenda Dameski zilizoandikwa kwa masinagogi , ili akiona watu wa njia hii waume kwa wake awafunge na kuwaleta Yerusalemu , Hata alipokuwa akisafiri ikawa anakaribia Dameski , Ghafla akamwangaza kotekote Nuru kutoka mbinguni , Akaanguka chini akasikia sauti ikimwambia, Sauli, sauli mbona waniudhi? , Akasema uu nani wewe Bwana? Akasema mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe, lakini simama uingie mjini nawe utaambiwa yakupasayo kutenda. Matendo 9:1-6

Simulizi: Mtu jina Sauli mtu jeuri na ni myahudi, Alikuwa tokea mwanzo akilitesa na kuliudhi kanisa na waumini . Siku moja akiwa njiani akiwateka wayahudia wengi kuwapeleka Yerusalemu , Mungu

akamtokea kwa mwanga wa Radi na kumwambia " Sauli sauli mbona waniudhi mimi? Sauli akajibu, Uu nani Bwana " Mimi ni Yesu unayemwuudhi , Tazama Nenda hata Mjini utaambiwa la kufanya, Sauli akaamka katika nchi na macho yake yalipofumbuka hakuona kitu , na wale waliosafiri na wakatulia kimya , wakiisikia sauti na hawaoni kitu , nao wakamshika mkono wakamleta mpaka Dameski, akawa siku tatu haoni wala hanywi kitu.

Nukuu: Sauli aliamini kwamba yeye ni mtu mkamilifu na akalazimika kuwazuia na kuwatesa wafuasi wa Yesu kristo, (walioitwa wafuasi wa njia ile) na alikuwa akiwapiga wao, na pia alikuwa akiomba Ruhusa kutoka kwa wakuu wa Dini kwenda barabarani mbali na kuwauwa wafuasi wa kristo Yesu (Wanawake kwa wanaume ) wanaotoka Yerusalemu na kuwajeruhi wao, sio tu hao wakuu wa Dini wanamruhusu sauli peke yake pia wanampa na askari wa kwenda naye, Sauli akaanza huko Damaska kwa siku ya sita , Damaska ni mji mkuu na nzuri na ilionekana huko mitume wengi wakiwa pale kama stephano waliyemuuwa kwa mawe.

Wakati anakaribia Dameski ,Ghafla Sauli akazungukwa na mwanga ukiambatana na Radi kali, Mwanga ulikuwa unawaka kuzidi mwanga wa jua, akasikia maneno ikizungumza naye yakisema kwamba, Sauli! Sauli! mbona waniudhi? Akasema u nani wewe Bwana? Sauti ya pili ikabadilisha maisha ya Sauli, Naye akasema mimi Mdimi huyo Yesu unayemwuudhi wewe , Sauli akaogopa sana, akauliza akitetemeka na kuuuliza , Nini hilo unalotaka kulitenda kwangu? Na Yesu akamwagiza yeye kwenda Dameski (karibu na mji) na hapo utafunguliwa,

Maandiko: Basi palikuwapo Dameski mwanafunzi jina lake Anania , Bwana akamwambia katika maono , Anania, akasema mimi hapa Bwana, Bwana akamwambia simama enenda zako katika njia iitwayo Nyofu , ukaulize katika nyumba ya Yuda mtu aitwae Sauli wa Tarso, maana angalia anaomba, Naye amemwona mtu jina lake Anania , akiingia na kuweka mikono juu yake na kumwombea apate kuona tena , Lakini anania akajibu akamwambia , Bwana nimeskia habari za mtu huyu kwa watu wengi mabaya aliyowatendea , watakatifu wako Yerusalemu , hata hapa ana Amri itokayo kwa wakuu wa makuhani, awafunge wote wakuitiayo jina lako, Lakini Bwana akamwambia Nenda tu maana hichi ni Chombo Kiteule kwangu alichukue jina langu Mbele ya mataifa. Na wafalme na wana wa Israel, maana nitamwonyesha yaliyo mengi yatakayompasa kuteswa kwa ajili ya jina langu. Matendo 9:1-16

Huko Dameski palikuwa na mtu jina lake Anania amabye Mungu alizungumza naye kwa maono na kumwambia aende mahali pale sauli anaomba, anania akajibu na kusema kwamba huyo mtu amekuwa akiwatesa wakristo na kasababisha madhahara makubwa kwa wakrsto na waumini wengi na akiwa na ruhusa kutoka kwa wakuu wa dini kwamba awajeruhi wale wanaoliitia jina lako.

Mungu akamwambia Anania kwamba , Nenda kwa huyu mtu maana ni chombo changu kiteule ili alichukue jina langu mbele ya mataifa na wafalme na wana wa Israel, nitamwonyesha yalio mengi yampsayo kufanya kwa ajili ya jina langu .

Basi anania akatoka na kuingia katika nyumba alipo na kuweka mkono wake juu ya sauli na kusema , Ndugu sauli , Bwana amenituma Yesu, Yule aliyekutokea katika njia ulioijia upate kuona tena na ukajazwe Roho mtakatifu, Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona akasimama, akabatizwa, kwa utaratibu wa Neno la Mungu.

Nukuu: Kule Dameski mtu aliyekuwa anaitwa Anania alitokewa na maono ya Mungu, Mungu akamtokea aende kwa sauli. Mungu pia alimwambia yeye kwamba sauli ni kipofu na anaomba na anakusubiri wewe uende pale na ndipo macho yake yatakapofunguliwa , Lakini anania akawa hataki kusikiliza sauti ya Mungu , Akasema ! Bwana! Hakuelewa, kwamba huyu Mtu atanisababishia taabu, Nukuu kwamba kwamba huyu mtu ni Mtu wa kupigana ambae hakudhaniwa kukaa na watu, Lakini Mungu akamtumia anania.

Wajibu: Utii pia huambatana na Imani: Wakati mtu anaomba ampokee Yesu, Roho mtakatifu kwake hamwachi, atamjaza na kuwa mtu wa kristo kwa njia ya Roho Mtakatifu , Huyo mtu sio yule tena , kwani mtu anakuwa kiumbe kipya na kuanza kwenda chini ya uongozi wa Roho mtakatifu.

Nukuu : Mungu hawaiti tu watu na kuwaokoa lakini pia anawaita ili awatengeze kweli . hapa Mungu alimwita Sauli, Mtu aliyefundishwa maandiko ya Agano la kale, na kumpa yeye mwanga kwamba atakuja kuwa mmisionari mkubwa kwa watu wote wale ambao sio watoto wa Ibrahim, na alichaguliwa kwa ajili hiyo ,yeye ni familia ya watu wanaoishi Asia, (Hivyo mwanzo alimpofusha yeye na baadaye aweze kurejeshewa Nuru , Pamoja na kwamba Paulo alitesa waumini, Lakini Anania alimwamini Mungu, na kulitii Neno lake,

Swali: Aanania alikuwa ni mwamini mzuri tangu utoto wake na aliagizwa na Mungu kumsaidia Sauli, Agizo ambalo lilikuwa linaweza kusababisha madhara kwa anania, wewe ungependa kuwa kama Anania uenende kwa mtu yeyote Ambaye Mungu atakuagiza?

SIMULIZI SEHEMU YA 13: PETRO AONA KAPU LIKITEREMKA KUTOKA JUU MBINGUNI LENYE WANYAMA NAJISI. Matendo 10:9-16.

Maandiko: Hata siku ya pili walipokuwa wakisafiri na kuukaribia mji , petro alipanda juu darini , kwenda kuomba yapata saa sita ya mchana, akaumwa na njaa sana akataka kula, lakini walipokuwa wakiandaa roho yake ikazimia, akaona mbingu zimefunuka na chombo kikishuka , kama nguo kubwa , inatelemshwa kwa pembe zake nne hata nchi, ambaye ndani yake walikuwemo aina zote za wanyama wenye miguu minne na hao watambao na ndege wa Angani , Kisha sauti ikamjia kusema , ondoka petro uchinje ule, Lakini petro akasema hasha Bwana kwa maana sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au Najisi , Sauti ikamjia mara ya pili ikimwambia, vilivyotakaswa na Mungu usiviite wewe Najisi, Jambo hili likatendeka mara tatu kisha chombo kile kikapokelewa tena mbinguni. Matendo 10-9-16.

Simulizi: katika mji wa kaisaria alikuwepo mtu alikuwa akiitwa kornelio, ambaye alikuwa akida wa kikosi kilichoitwa kiitalia, Yeye na familia yake walikuwa wakimwabudu Mungu, Alikuwa ni mtu mtauwa na kuwapa maskini sadaka nyingi , alikuwa ni mtu wa maombi, mnamo saa tisa kamili ya mchana aliona maono na malaika wa Bwana akazungumza naye akisema , Kornelio maombi yako na sadaka zako zimefika mbele za Mungu, mtume mtu na aende kwa petro akamwite aje kwako. “wakati huo huo Mungu alimwandaa petro kuja kwa kornelio. Mungu alijua kwamba petro ana tatizo kuhusu mataifa na kwa Mungu wake , ikawa shida machoni pa Petro,. Mungu anajua tokea mwanzo kwamba mataifa yote watakwenda kumgeukia yeye, lakini watoto wa Ibrahim wao wanajua kwamba wokovu ni wa kwao tu, watamgeukia yeye bali watoto wa Ibrahim walijua na kufikiri kwamba Mungu atawapokea wao tu, Mungu akamtumia Petro bila yeye kutarajia .

Siku moja mchana (muda wa mchana kama ilivyo Desturi ) simon petro alikuwa mle chumbani darini akiomba , akaona Mbingu zimefunuka na chombo kikishuka kama Nguo kubwa inatelemshwa kwa pembe zake Nne, hata Nchi, Ambao wamejaa aina zote za wanyama ambao petro anajua ni haramu kuliwa, kisha sauti ikamjia ikisema Ondoka Petro uchinje ule, Lakini petro akasema , hasha Bwana kwa kuwa sijakula kamwe kitu kilicho kichafu au Najisi.

Wajibu wetu: kama wakristo, Lazima na sisi tuambatane kwa fundisho la Neno la Mungu na sio kufungwa na Desturi ambayo inapingana na Neno la Mungu, na ndio maana ni muhimu wakristo wote pamoja na kanisa ,lifundishe maagizo ya Mungu lakini pia kuwa na Biblia wewe mwenyewe au watoto wako wanaweza wakakusomea au mtu mwingine anayejua kutafsiri anakutafsiria na kukufundisha, Na hivyo utaweza kukua kama mtoto wa Mungu anayefundishika, Jifunze Neno, Heshimu Neno, Umeona

hapo simoni petro alipojibu “Hapana Bwana” Yeye ni mtu na ni kiongozi wa njia na mwenye Tabia za Yesu ambae alikuwa anasema hapana kwamba Yesu amekuwaje Bwana kwake na ndipo Petro anakataa .

Nini inafanya kitu kuwa Najisi au isiwe Najisi,? Ni sheria. (Walaw 20:25-27) Ina umuhimu gani? Ona hili jambo linatupa uhakika na ujasiri wa utakatifu wa kiungu aliyegawa yeye mwenyewe kwa watu (kuanzia Abraham,) aliyeitwa Baba wa imani, “ Huu ni muda mzuri wa wakufunzi kujua kwamba Tangu kabla ya Abraham wote tulikuwa mataifa , Nini imekuwa Ngumu kwa petro? Alijifunza katika maisha yake yote kwamba wote ambao sio watoto wa Ibarahimu ni wacahafu, na hawataamini , hata na hivo alijua kwamba ni ngumu kuwa nao kukaa nao, kugusana nao, na kushirikiana kwa chakula kwa sababu wanaweza kumnajisi. Na hapo petro anauliza kwa vipi wokovu unaenda kwa mataifa, kwanini ilitakiwa afanye hivyo? Wakristo wanatakiwa wawe makini, na sio kuamini kwa jinsi petro alivyofanya na kutazama kwa watu wengine, nini ilibadilisha mtazamo wa petro ni na mawazo yake? Hapana! Ni Neema ya Mungu tu ikiambatana na utii, Mungu aliita kipi ni kisafi,

Swali: Je Wewe ni kama Petro? Unaruhusu Desturi zako na mila zako? Kwamba utaweza kuingiza kwenye kusudi la Mung? Je unafundishika? Utachukua hatua gani kama mmojawapo na kufanyia kazi kile uliyoagizwa?

SIMULIZI SEHEMU YA 14: KORNELIO Matendo 10:1-8,24-48

Maandiko: “Palikuwa na Mtu kaisaria Jina lake Kornelio akida wa kikosi kilichoitwa kiitalia , mtu mtauwa mchaji wa Mungu , yeye na nyumba yake yote naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi na kuwapa watu Daima, akaona katika maono waziwazi, kama saa tisa ya mchana, malaika wa Mungu akimjia na kumwambia,Kornelio, akamtazama sana akaogopa akisema kuna nini Bwana? Akamwambia Sala zako na sadaka zako zimefika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu, sasa basi peleka watu Yafa ukamwite aitwae simoni petro”

Simulizi: Kwenye mji mmoja kulikuwa na akida mmoja aliyeitwa Kornelio, ambae alikuwa na cheo kubwa katika jeshi Yeye na Familia yake walikuwa wakimwabudu Mungu , alikuwa akitoa sadaka nyingi kwa wasiojiweza .

Siku moja yapata saa tisa mchana, aliona maono na malaika wa Bwana akizungumza naye , “Kornelio” Maombi yako na sadaka zako zimefika mbele za Mungu , mtume mtu aende kwa petro akamwite aje kwako, Petro alikuwa nyumbani akiomba kutokana na yale Mungu amemwonyesha na kwamba Roho mtakatifu alimwonyesha kwamba kuna wanaume watatu wanakuja kwako, na wako watatu, wakimweleza tumekuja , Na tunakuomba tuende kwenye Nyumba ya kornelio, na hapo akaungana nao.

Maandiko: Hata Petro alipokuwa akiona shaka ndani ya Nafsi yake, maana yake nini maono hayo aliyoyaona, wale watu waliotumwa na kornelio, wakiisha kuuliza nyumba ya simoni, wakasimama mbele ya mlango , wakaita wakauliza mtu aitwae simoni petro anakaa humo, na petro alikuwa akiyafikiri yale maono, Roho akamwambia wako watu watatu wanakutafuta , Basi ondoka ushuke ufuatane nao , Usione tashwishi kwa maana ni mimi ndiye niliyewatuma , Petro akawashukia wale watu akanena , mimi ndiye mnayemtafuta mmekuja kwa sababu gani? , wakasema kornelio akida mtu mwenye haki , mchaji wa

Mungu aliye na sifa njema kwa taifa lote , la wayahudi , alionywa na malaika mtakatifu kutuma watu kwako ,uende nyumbani kwake apate kusikiliza maneno kwako (Matendo 10:17-22)

Simulizi: Walipofika kule , watu wengi wakakusanyika pamoja . na kornelio akamweleza Petro hayo maono , na kwanini alimwita petro, kwa hiyo wote waliokuwepo pale waliskia kwamba Bwana amekupa nini useme kwetu.
Maandiko: " Mara nikatuma watu kwako, nawe umefanya vyema kuja , Basi sasa sisi sote tupo hapa mbele za Mungu, tupate kuyasikiliza maneno yote, uliyoamriwa na Bwana, Petro akafumbua kinywa chake , Akasema! Hakika, natambua ya kuwa Mungu hana upendeleo, bali katika kila taifa kila mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye, Neno lile alilowapelekea wana wa Isaraeli, akihubiri habari njema ya amani kwa Yesu kristo (yeye ni Bwana wa wote)" (Matendo 10:33-36)
Simulizi: Nini kilifuata, Ni Simon petro aliwahubiri habari njema kwa kornelio na watu wote waliomo pale chumbani, alianza na ubatizo wa Yohana, na kuendelea kuishi maisha matakatifu, na kuepukana na uovu kwa kifo chake kwa kusulubiwa na kufufuka kwake , Petro alimalizia kwa kuwaalika na kuwaagiza kwa usahihi habari za neema kubwa ya Mungu, na wokovu kwa kila mmoja atakayemwamini Yesu kristo kwamba atapokea msamaha wa Dhambi
Maandiko: Petro alipokuwa akisema maneno hayo, Roho mtakatifu akawashukia wote, walioliskia lile Neno. Na wale waliotahiriwa walioamini ,wakashangaa watu wote walikuja pamoja na Petro kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu , kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha na kumwazimisha Mungu , Ndipo petro akajibu, ni nani awezae kuzuia maji, hawa wasibatizwe watu waliopokea Roho Mtakatifu kama sisi,? Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo , Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha. (Matendo 10:44-48)
Simulizi: Hivyo Petro akaanza kumuhubiri Yesu , na Roho mtakatifua akaja juu yao wote waliosikia ujumbe huo pamoja na wote walioamini wakabatizwa.

Wayahudi wakashangazwa na mabadiliko ya mataifa, kwani imekuwa kama ile siku ya pentekoste , Petro akauliza , nini kitakachonyima watu hawa wasibatizwe? Wamepokea Roho mtakatifu kama na sisi pia, na ndio watu wa kwanza kwa mataifa kupokea Roho Mtakatifu na kubatizwa wawe familia ya Mungu. Injili nayo wamepewa mataifa?
Nukuu: Tafadhali Onyesha tofauti kati ya simoni Petro na Kornelio, Simoni Petro ni wa uzao wa Ibrahimu alisema, hapana mara tatu, wakati kornelio ni mataifa asiyeamini nao wakasema ndio haraka sana iwezekanavyo, kwamba ilikuwa ni ujasiri wa petro iliwafanya wawe na utii na hiyo inafanya kazi katika maisha yetu pia.
Kuhusiana na wale wanaoongea kwa ndimi zao: Mungu alimpa ujasiri kupitia Roho mtakatifu aliposhuka juu yao walipoamini, Huwa hatuamini kwamba kila mtu atakayetubu na kumwamini atakuwa na ujasiri hivyohivyo, hakuna mtu awezae kuacha dhambi pasipo Neema ya Mungu.
Wajibu: Haitoshi kwamba mwanadamu ni mtu mwema au ni mwenye haki, Mwanadamu anahitaji msamaha wa Dhambi , na kwamba ni mmoja tu, ndiye anayeweza kufanya hayo, Ni Yesu kristo mwana wa Mungu. Mungu hutumia watu wenye hekima kuwaambia watu wengine kuhusu habari za Yesu
Swali: Uko tayari kutanagza habari njema kwa wengine , haijalishi wana utofauti gani na wewe?

SIMULIZI SEHEMU YA 15: BAA LA NJAA KATIKA NCHI:

( mitume watuma sadaka zao kuwasidia wale wasio na chakula) Matendo 11:27-30

Maandiko : Siku hizo hizo mitume walitelemka kutoka Yerusalemu hata Antiokia, na tulipokusanyika akasimama mmoja wao jina lake Agabo, akaonyeshwa na Roho mtakatifu, kwamba njaa kubwa itakuja karibu, katika Dunia Nzima , nao ikatukia katika siku za klaudio, Na wale wanafunzi kila mtu kwa kadri ya alivyofanikiwa wakaazimu kuleta kupeleka msaada kwa Ndugu zao waliokaa Uyahudi , wakafanya hivyo wakawapelekea wazee kwa mikono ya Baranaba na sauli. (Matendo: 11:27-30)

Simulizi: kutokana na kanisa la Mungu lililoanza huko Antiokia, hivyo ilimlazimu Barnaba (Watu wenye uzoefu wa kufundisha,) watoke Yerusalemu wakawaweka viongozi wa kanisa pale, walipooona ongezeko kubwa, walilazimika kwenda Tarso kumtafuta Sauli, ambaye siku moja alipokuwa njiani akielekea Dameski aliitwa Paulo,(Matendo 13:9) Paulo alikuwa msukumo na utayari wa kuhubiri Injili kwa mataifa , hapo Paulo akaanza huduma yake kule Antiokia , wakati huo walikuwepo wahudumu wa wanabii huko Yerusalemu jina lake Agabo ,alimwambia njaa kubwa imetokea na waumini wengi hapa Yerusalemu wamekuwa na uhitaji mkubwa kutokana na umaskini wao . Na hii ilianza siku hizo hizo za Sauli , kanisa likapanga kutoa misaada na sadaka na kuwatumia Sauli na Barnaba. Hivyo waumini wapya walitakiwa kuonyeshwa upendo huko Yudea na kukusanya hela na kuwatumia na kuwasadia mpaka njaa itakapoisha , Kwani hawakufanana na wao na hawakujua , walielewa pia kwamba kuwasaidia watu ndio chanzo kikubwa cha kuteka mioyo yao.

Nukuu: Hili ni jambo kubwa katika nchi ya wamasai , Israeli pia walipigwa na janga la njaa na ukame .

Wajibu: Kwa sababu waumini wote ni sehemu ya Familia ya Mungu , Sisi tunaimarishwa kwa kuona watu wanabadilisha mioyo yao na kuwa tayari kwa ajili ya Mungu ili tutumike lazima tukawaone.

Swali: wakati Paulo akiishi Tarso kwa miaka kadhaa baada ya kuitwa kwake , alitambua Dhambi zake alipokua akilitesa kanisa , kwamba Mungu amemsamehe, Kumbuka Paulo yeye ndiye aliyeshikilia mawe za kumuulia Stefano, Una unaamini kwamba Mungu anaweza kukusamehe wewe na kukutumia wewe?

SIMULIZI SEHEMU YA 16: PETRO AKIWA GEREZANI NA MALAIKA AFUNGUA MILANGO

Matendo 12:1-12

Maandiko: “Panapo majira yale yale Herode mfalme akanyoosha mikono yake kuwatenda mabaya baadhi ya watu wa kanisa, Akamuuwa yakobo Ndugu yake Yohana kwa upanga na akiona ya kuwa imewapendeza wayahudi, akaendelea akamshika na Petro, siku hizo zilikuwa siku za mikate isiyochachwa , alipokwisha kumkamata akamweka Gerezani akamtia mikononi mwa vikosi vinne vya askari wanne wanne wamlinde, akitaka baada ya pasaka wamtoe na kumweka mbele ya watu.” (Matendo 12:1-4)

Simulizi : (Wakati huo) Herode( Agripa) Mfalme alianza kulitesa kanisa, Alimchukua Yakobo mmojawapo kiongozi wa kanisa akamuuwa , na alipoona kwamba amewapendeza wakuu wa Dini , akamchukua na Petro na kumfunga Gerezani na akapanga kumuangamiza baada ya sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu. Lakini wakati Petro akiwa Gerezani, Kanisa likaomba kwa ajili yake mchana na usiku.

Maandiko: “Basi Petro akalindwa Gerezani Nalo kanisa likamwomba Mungu, kwa juhudi kwa ajili yake, hata wakati herode alipotaka kumtoa ,usiku uleule petro alikuwa analala katikati ya maaskari wawili wamefungwa minyororo miwili, walinzi ndani ya Mlango wakailinda Gereza, Mara malaika wa Bwana akasimama karibua naye , Nuru ikamulika mule chumbani akampiga Petro ubavuni , Akamwamusha akisema! Ondoka upesi, Minyororo yake ikamwanguka mikononi, Malaika akamwambia Jifunge kavae viatu vyako .akafanya hivyo. Kisha akamwambia jivike nguo zako ukanifuate. Akatoka Nje akamfuata wala hakujua ya kuwa ni kweli yaliyofanywa na malaika bali alidhani kwamba anaona maono. “(Matendo 12:5-9)

Simulizi: Panapo usiku mmoja kabla Herode hajaenda kumwadhibu Petro, wakati alipofungwa gerezani kwa minyororo na kuwekewa walinzi , Panapo usiku wa manane , Kumbe, Malaika wa Bwana akaja na kumulika kila sehemu , Malaika akamwamusha petro na kumwambia , Amka ,vaa mavazi yako Twende, Minyororo ikakatika na milango zikafunguka na Petro akatoka Nje, Malaika akatembea naye wakapita geti zote, mpaka na lile geti kubwa la kuingilia nao wakapita, na geti zilikuwa zikijifungua zenyewe,
Nao walipopita Geti la Mwisho na kuingia mjini , malaika akaondoka, Ndipo Petro akatafakari kilichotokea akiwa katika hofu ndipo akajua kwamba Bwana, na hapo akajua kwamba ni Bwana ndiye aliyemweka huru.
Maandiko: Na walipopita lindo la kwanza na la pili, wakaja hata mlango wa Chuma wa kuingilia mjini, ukawafungukia wenyewe, wakatoka Nje wakapita katika njia moja, mara malaika akamwacha, Hata Petro alipopata fahamu akasema, sasa nimejua yakini ya kuwa Bwana amempeleka malaika wake na kunitoa katika mkono wa Herode na katika kutazamia kote kwa Taifa la wayahudi. (Matendo 12:10-11)
Simulizi: Akaenda nyumbani kwa mariamu (Mamaye Yohana) akagonga mlango, na watu wengi waliomwani Yesu walikuwepo pale wakiomba kwa ajili yake , na Kijakazi Rhoda akaja kuchungulia malangoni na alipomhakikisha hakufungua mlango kwa ajili ya Furaha bali alipiga mbio na kuwaambia wengine kwamba ni Petro! na hapo wakiwa wanawaza kwamba ni petro? au malaika, wakafungua mlango na kumbe ni petro na wakamkaribisha ndani.
Maandiko: “ Na alipokuwa akifikiri haya akafika Nyumbani kwa mariamu, mamaye Yohana ambaye jina lake la Pili ni Marko, na watu wengi walikuwa wamekutana humo wakiomba naye alipobisha kilango cha Lango, kijakazi Jina lake Roda akaja kusikiliza alipoitambua sauti ya Petro hakukifungua Lango kwa ajili ya Furaha, bali alipiga mbio akaingia ndani, akawaambia kwamba Petro anasimama mbele ya Lango, wakamwambia una wazimu, lakini yeye akakaza sana, akasema ya kwamba ndivyo hivyo, wakanena ni malaika wake, Petro akafuliza kugonga, hata walipokwisha kumfungulia wakamwona, wakastaajabu, Naye akawapungia mkono wanyamaze , Akawaeleza jinsi Bwana alivyomtoa katika Gereza, akasema kampasheni yakobo na wale Ndugu Habari hizi, akaondoka akaenda mahali pengine” . (Matendo 12:12-17)
Rafu: Yakobo ndugu yake Yohana, ndiye mtume wa kwanza kuteswa na kuuliwa , na kifo chake kilijulikana sana. Ilisikitisha kwetu, lakini kwa wayahudi walifurahi kwani waliona wameshamnyamazisha na sasa yuko mbali nao , ilitokea kabla ya hapo na kwa muda, mtakatifu wa wayahudi, ni mmoja ambao wao walisherekea kufa kwake, Mfalme herode alimwona Yakobo kwamba kifo chake imekuwa furaha kwa watu wengi, hivyo akaamua kumuuwa pia na Petro, Alimwadhibu na kumtupa Gerezani na hiyo ilikuwa ni mara yake ya tatu kila mmoja katika hao wanne walinzi maalumu masaa 24 kwa siku, kwamba walinzi 16 kwa kila mtu ambao hawatakataa kuwauwa , naye akafungwa na walinzi wawili na walinzi wawili wengine walikuwa wakilinda lango upande herode anapotazamaga, ilikuwa sio rahisi kuepuka (labda yeye alikumbuka muda wakati mitume walipoepuka kutoka jela bila mlango kufunguliwa na mlinzi wa lango) akawa ameshtuka kiasi kwamba akifikiri wafungwa hawako ndani lakini kumbe wapo,
Matendo ya mitume 5:22)
Waumini wa kanisa waliposikia kwamba petro amefungwa Gerezani , walianza kuomba kwamba Jaribu hilo limwepuke na kupewa nguvu ya uvumilivu, (c.f 5:40) Lakini Roho Mtakatifu ana mpango tofauti, Panapo Usiku kabisa kabla ya kupambazuka katikati ya saa 4 na 6 ili kupambazuke, Bwana akamtuma malaika wake kwa petro akiwa mle ndani, petro alikuwa amelala, na hawezi hata kuhusu kesho kwamba itakuwaje kwake, malaika akamgusa petro na kusema , Amka! Chukua mavazi yako tuondoke .
Kwa vyovyote minyororo yaliyokuwa amefungwa petro zikadondoka ,Malaika akamwambia “Nifuate mimi toka kifungoni” Malaika akamwongoza petro .lakini Petro hakuelewa vizuri kilichotokea (Alidhani anaota) Lakini akamfuata malaika kama vile malaika alivyomwambia , Tazama geti zikaamuriwa zifunguke zenyewe, (kwa nguvu za Mungu) wakatoka nje, na baada ya hapo malaika akamwacha , alimwacha

akiwa huru na kifungo , Malaika akarudi kwa Mungu na ndipo petro akaelewa kilichotokea na hapo akarudi kwenye familia ya kanisa. ?

Wajibu wetu: Ni muda gani umeomba kwa ajili ya kitu na tukijua ndani ya mioyo yetu na kutoamini kwamba Mungu atajibu na endapo Mungu akifanya utashtuka? Mungu pia hujibu maombi yetu kama tukiomba kwa imani.

a) Wakati anasema " Subiri hata kama sio leo " Kwa hiyo anajibu kwa wakati wake na kwa njia nzuri b) Muda mwingine anajibu "Hapana" kwa sababu anajua kutupa sisi vile tuombacho na kipi sio nzuri kwetu na kipi ni kizuri c) Iko wakati anatujibu "Ndio" na hii itatusaidia sisi kutembea pamoja naye Lengo ni kujihudhurisha na kujifunza kujitosheleza na chochote Mungu atakapojibu kwa ndoto Nzuri (Filipo 4:11-12)

Mungu akamwambia petro asikosekane kwenye matimilisho na majukumu ya pasaka kila wakati , ikionyesha kwamba mipango yake ilikuwa imejiwekeza kwa wale walioamini na kumpokea Yesu Kristo mwana wa Mungu na Mungu bado ana mipango na wana wa Israel, bali sio kwa mila za watu wanaoona kuwa hii inakubaliwa kuliko Mungu mwenyewe

Swali: Luka aliandika hesabu, na aliandika kwa mtu ambaye alikuwa anajaribu kuelezea kumuhusu Yesu na kanisa, je unafikiri kwanini yeye alihusisha hadithi hii? Unafikirije kwanini petro alijishusha alipokuwa akisubiri kushtakiwa mahakamani? Je unaonaje petro alipoachiliwa gerezani aliadhirika kiasi gani katika maisha yake? Wewe ungefikiri nini kingekudhuru kulikuwa hakuna yaliotajwa kuhusu ulinzi uliofanyika unafikiri wao walifanya nini?

SIMULIZI SEHEMU YA 17: PAULO NA BARNABA ,WAPAKWA MAFUTA KWA KUHUBIRI NA KUPANDA MAKANISA Matendo 13:1-4,14:19-23

Maandiko: "Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana Ibada na kufunga , Roho Mtakatifu akasema , Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi hiyo niliyowaitia , Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao wakawaacha waende zao, Basi watu hao wakiisha kupelekwa na Roho Mtakatifu, wakatelemkia seleukia , na kutoka huko wakasafiri Baharini hata kipro." (Matendo 13:2-4)

"Lakini wayahudi wakafika toka Antiokia na ikonio, wakawashawishi makutano hata wakampiga kwa mawe, Paulo wakamburuta nje ya mji wakidhania kuwa amekwisha kufa , Lakini wanafunzi walipokuwa wakimzunguka pande zote akasimama akaingia ndani ya mji, na siku ya pili yake akatoka akaenda zake pamoja na Baranaba mpaka Derbe. Hata walipokwisha kuihubiri Injili katika mji ule , na kupata wanafunzi wengi , wakarejea mpaka Listra, Ikonio, na Antiokia, na kufanya imara roho za Wanafunzi na kuwaonya wakae katika Imani na ya kwamba imetupasa kuingia katika Ufalme wa Mungu, kwa njia ya Dhiki nyingi, na walipokwisha kuwachagua wazee katika kila kanisa na kuomba pamoja na kufunga, wakawaweka katika mikono wa Bwana waliyemwamini" (Matendo 14:19-23)

Simulizi: Baada ya Barnaba na Paulo kuleta matoleo Yerusalemu , na kuwapa viongozi wa pale alafu warudi Antiokia (Antiokia imekuwa kama sehemu ya kazi ya umisheni wao wa kanisa) kanisa likadumu chini ya Uongozi wa Roho mtakatifu huduma ya paulo na Barnaba ilikuwa ni huduma kubwa, Mungu ameweka kwao kwa ajili ya kanisa , Aliwafanya Mitume , watu wengi wakawa waumini katika safari yao, wengine ni wa Yerusalemu na wengine wa Mataifa , Sehemu za mijini injili ilihubiriwa. Wengine wakaanza kumpinga Paulo na Barnaba

Wakati wakihubiri na kufundisha huko Listra, watu wakawa wanasumbuliwa Wakamchukua Paulo wakimpiga kwa mawe na kumtaka yeye afe, Baadhi ya watu wakaja wakamchukua yeye kutoka pale , na

siku ya pili yake Paulo na Barnaba wakaenda kwenye mji mwingine , (Derbe) wakawa wanaenda mji hadi mji kumuhubiri Yesu na kuanzisha makanisa kila mahali ambapo watu wameamini,
Maandiko: " Kutoka huko wakahubiri kwenda Antiokia, huko ndiko waliko ombewa Neema ya Mungu kwa ile kazi waliokwisha kuitimiza ,hata walipofika wakalikutanisha kanisa ,wakawaeleza mambo yote aliyoyafanya Mungu pamoja nao na ya kwamba amewafungulia mataifa mlango wa Imani, wakaketi huko wakati usiokuwa mchache pamoja na wanafunzi, " (Matendo 14:26-28)
Simulizi: Kanisa likaendelea kukua, likapata nafasi, Paulo na Barnaba wakaenda mji kwa mji kueneza habari njema hata kwa njia ya Yerusalemu , walipokelewa kwa mikono na kwa furaha nyingi nao wakaanza kueleza yale Mungu amefanya kupitia wao
Wajibu : Tukio hili ilifanyika kwao na sisi tupate ujasiri wa kutangaza habari njema , kuleta faida kwa Yesu kristo. tuelewe kwa sababu wengine walikuwa na miungu yao na watatakiwa wajisalimishe kwa Yesu kristo. Tuanapopeleka ujumbe wa Neno la Mungu kwa Watu hata hakuna mwitikio lakini Mbegu itakuwa pale milele.
Swali: Maoni yako ni yapi, Yesu anamaanisha nini anaposema, Heri Ninyi wanapowashutumu, na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya na uongo kwa ajili Jina langu (Mathayo 5:11-12) unadhani utakuwa Tayari kupokea na kuwa tayari?

SIMULIZI SEHEMU YA 18:PAULO NA SILA GEREZANI (Matendo 16:22-30)
Maandiko: "Ikawa Tulipokuwa tukienda mahali pale pa kusali , kijakazi mmoja aliyekuwa na pepo wa uaguzi, akatukuta aliyewapatia bwana zake faida kwa kuagua , akamfuata Paulo na sisi akipiga kelele, akasema watumishi wa Mungu aliye juu, wenye kuwahubiria njia ya wokovu , akafanya hayo siku nyingi lakini Paulo akasikitika ,akageuka akamwambia Yule pepo, Nakuamuru kwa jina La Yesu Kristo mtoke huyu akamtoka saa ile. Basi bwana zake walipoona ya kuwa tumaini la faida yao limewapotea,wakawakamata Paulo na sila wakawakokota mpaka sokoni mbele ya wakuu wa mji". (Matendo 16:16-19)
Simulizi: Paulo na sila walikuwa wakitembea mji kwa mji na wakihubiri habari njema za Yesu na mwitikio wa watu ukazidi kuongezeka , siku moja walikuwa wakienda mahali kuomba, Na Tazama kulikuwa na binti Mmoja mwenye mapepo ya utambuzi, na aliyewateka matajiri wengi wakimfuata yeye na kumkubali, Alipowaona akina Paulo, akasema hawa ni Watumishi wa Mungu aliye juu, na wanahuburi njia ya wokovu, Paulo akashangazwa sana, akamkemea lile pepo na kuamuru limtoke huyo mtu. Wale waliokuwa wakifuatana naye wakakasirika na kuwakamata wakina Paulo na kuwaweka penye mamlaka na kuwafunga wasihubiri, wakachapwa na kutupwa gerezani , na walinzi wakaamriwa wawalinde wasitoroke
Maandiko: Walipokwisha kuwapiga mapigo Mengi ,wakawatupa Gerezani wakamwamuru mlinzi wa Gereza awalinde sana,Naye akiisha kupata amri hii, akawatupa katika chumba cha Ndani, akawafunga miguu kwa mikatale, Lakini panapo usiku wa manane Paulo na sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza, Ghafla pakawa tetemeko kuu la nchi, Hata Misingi ya Gereza ikatikisika, na mara hiyo milango ikafunguka, Vifungo vya wote vikalegezwa. (Matendo 16:23-26)
Simulizi: Wakawekwa gerezani nao wakafungwa kwa minyororo, panapo usiku wa manane Baada ya kuchapwa na kutupwa Gerezani , Paulo na sila walizidi kuimba na kumsifu Bwana, wale wafungwa wengine wakawa wakiwasikiliza na tazama kukasikika tetemeko kubwa, na mara milango ya gereza zikafunguka na minyororo zikakatika.
Maandiko: Yule mlinzi wa Gereza akaamuka, naye alipoona ya kuwa malango wa Gereza Umefunguka, alifuta upanga ,akataka kujiua,akidhani ya kuwa wafungwa wamekimbia, na Paulo akapaza sauti yake

kwa Nguvu akisema ,usijidhuru kwa maana sisi sote tuko hapa, akataka Taa ziletwe, akaruka ndani akitetemeka kwa Hofu ,akawaangukia Paulo na Sila, Kisha akawaleta Nje akasema Bwana zangu, Yanipasa Nifanye nini nipate kuokoka? Wakamwambia Mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka pamoja na Nyumba yako.

Simulizi: Askari wa Gereza alipoamka na tazama milango zote ziko wazi, akashtuka sana kwani alijua kwamba wafungwa wametoroka na wasipoonekana atauliwa yeye, na ndipo Paulo akamwita kwa sauti na kumwambia ,Usijiuwe kwani tuko hapa sote, hatujaondoka, ndipo Yule mlinzi wa Gereza akaanguka miguuni pao, na kuwaambia nifanye nini nam niweze kuokoka? Na Ndipo Paulo akamjibu " Mwamini Bwana Yesu Kristo nawe utaokolewa wewe na nyumba yako yote, naye akababtizwa usiku ule ule .

Wajibu: hamna mtu ajuae wakati wa Mungu wa kumwokoa mtu , Hivyo ni vema tuwe na ushirika kamilifu na Bwana, wakati wote ili kwamba Roho mtakatifu atutumie katika kuhubiri Injili kwa hali yeyote kwa uongozi wake na utendaji wa kazi wakati wowote, sehemu yeyote hata gerezani, Kikubwa ni kuwa makini na uongozi wa Roho Mtakatifu na kuwa watiifu kwake.

Swali: katika nchi nyingi , wakristo wanateswa na kuuliwa eti kwa sababu wanasema ni Wafuasi wa Yesu Kristo, wao wangefanyaje badala ya hili?

Kulikuwa kuna mtu aliyemuuliza mwingine , nani huyu anayelaumiwa kwa ajili ya ushuhuda , wewe ungependa kuhudumu katika njia hii?

SIMULIZI SEHEMU YA 19 –PAULO NA SILA WAENDA MJI KWA MJI

Matendo 17:1-12

Maandiko: "Wakiisha kupita kati ya Amphipoli, na Apolonia wakafika Thesalonike, ambapo palikuwa na sinagogi la wayahudi, na Paulo kama ilivyokuwa Desturi yake , akaingia kule walimo akahojiana nao ,kwa maneno ya maandiko sabato tatu, akiyafunua na kuwaelekeza ya kwamba ,ilimpasa kristo kuteswa na kufufuka katika wafu ,na ya kwamba Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari zake ndiye kristo , wengine miongoni mwao wakaamini wakashikamana na Paulo na sila na wayunani waliomcha Mungu, wengi sana na wanawake wenye cheo sii wachache, na wayahudi wakaona wivu wakajitwalia watu kadha wa kadha katika watu ovyo wasio na sifa njema na wakawakutanisha mkutano wakafanya Ghasia mjini , wakawaendea watu wa nyumba ya Yasoni, wakataka kuwapeleka mbele ya watu wa mji " (Mado 17:1-5).

"Mara hao Ndugu wakawapeleka Paulo na sila usiku hata Beroya, na walipofika huko wakaingia katika sinagogi la wayahudi, watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno katika unyofu wa moyo,wakayachunguza maandiko kila siku waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo? Basi watu wengi miongoni mwao, wakaamini na wanawake wa kiyunani wenye cheo na wanaume sii wachache," (Matendo 17:10-12)

Simulizi: Huduma ikaendelea kukua , na paulo na sila wakasafiri kama kawaida yao kwenda mji hadi mji na kuzidi kuhubiri, kufundisha na kutangaza habari njema , miji mingine wameskia ujumbe wao na wengi wamepokea lakini kuna sehemu zingine ilikataliwa, na iliwalazimu watoke nje ya hizo miji, wakati mwingine wanapigwa na kuwekwa kifungoni,

Baada ya Huduma yao huko filipi (Paulo akamwacha Luka huko kwa ajili ya huduma ya kanisa )Paulo na wanawake waliokuwa wakiishi nje ya thesalonike , maana mjini kulikuwa mbali, 160.9kilometers=mile100) ni umbali mrefu hivyo Paulo anatumia meli na farasi kusafiria, wakiwa safarini wakapitia baadhi miji kuhubiri habari njema za Yesu kristo, walipofika Thesalonike Paulo akawa kwenye Masinagogi, kwa takriban wiki tatu, akiwaambia wanaume wa pale Habari Njema za Yesu, wanaume wengi na wanawake walikubali kumfuata Yesu na kufanyika watu wa Njia ile , kwa ujumla watu wengi wakafanyika waumini hivyo Paulo na wale wote aliokuwa nao wakashutumiwa kwa kuleta mapinduzi , wayahudi wa Dini wakamnenea Paulo uongo kwa vitu ambavyo sio za kweli,wakazidi kumpinga, wakawa wakijifanya

kwamba ni watu wazuri ili waweze kumkamata Paulo kwa urahisi, lakini hawakufanikiwa kumkamata Paulo, au mmoja miongoni mwao, Nao wakamtuhumu kimakosa Jason, ambaye Paulo alikuwa kwake ,lakini mamlaka haikuwaadhibu wao , ikatia moyo Paulo alipotembelea mji uliofuata (Berea) akijihusisha kiujumla toafauti na alivokuwa Thesalonike.
Wajibu: Tunatakiwa tujulikane kwamba sisi ni wajumbe, Ni Roho Mtakatifu pekee mwenye uwezo wa kusisitiza na kuwaokoa wale wataokapokea ujumbe tunajua kabisa kwamba Mungu ametuokoa ili atangaze Neno lake kupitia sisi.
Swali: Je unaposhutumiwa na kunenewa uongo je? Utawezaje kupambananayo? Inatushangaza wayahudi kutoka Thesalonike wakisafiri umbali mrefu kutoka Berea 96.5km =mile 60 wakipinga mafundisho ya Paulo wakisema kwanini haya? Je unahitaji imani kubwa kuwaambia watu ambao wanakataa Injili kuliko kuwaambia watu wanaopokea injili? Je ungejiskiaje? Wakati unapowaambia watu wajifunze zaidi na kuifuata injili kwa ubora , matendo yenu yatakuwaje baadae?

SIMULIZI SEHEMU YA 20: PAULO NA MUNGU ASIYEJULIKANA-Matendo 17:16-34
Maandiko: “Paulo alipokuwa akiwangojea kule Athene , na kuona kwamba mji umejaa masanamu, roho yake ilichukizwa sana ndani yake, Basi katika sinagogi akahojiana na wayahudi na waliomcha Mungu na wale waliokutana naye sokoni kila siku.” (Matendo 17:16-17)
Paulo akasimama katikati ya Areopago akasema enyi watu wa Athene, katika mambo yote naona ya kuwa ninyi ni watu wa kutafakari sana Mambo ya Dini, kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko, kuyaona mambo ya Ibada yenu naliona Madhabahu iliyoandikwa maneno haya KWA MUNGU ASIYEJULIKANA ,Basi mimi nawahubirini habari zake yeye ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua , (Matendo 17:22-23)
Simulizi: Nao wakaendelea kutangaza habari njema , nao wakaja Athene, wakiwa wakipita mji hata mji, wakaona sanamu na mifano ya miungu mbalimbali, wakaenda mahali pa ukumbusho wakaandika juu yake Mungu asiyejulikana. Ikawa jambo la kushangaza kwa Paulo, na kusema kama wamebakiza miungu mingine ,hivyo ikawa ni kwa ajili hiyo, Paulo alichukizwa na kwenda kwenye sinagogi la wayahudi na kuanza kuwaambia na kuhubiri kwao, wao wakadhani kwamba ni mtu aliyesoma sana wakawa na hofu kutokana na jinsi walipomsikia juu ya (Mungu mpya) amabaye Paulo alikuwa akiwaambia , mwishoni wakawa pamoja mahali pamoja na Paulo akaanza kuwaeleza Juu ya huyo Mungu wao asiyejulikana na kusema, Mimi nimekuja kuwaeleza kuhusu hilo na Mungu asiyejulikana mumuache.
Maandiko: Mungu aliyeufanya ulimwengu, na vitu vyote vilivyomo ,yeye kwa kuwa ni Bwana wa Mbingu na Nchi hakai katika hekelu zilizojengwa kwa mikono, wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu , kana kwamba anahitaji kitu chochote , kwa maana ndiye anayewapa watu uzima na pumzi na vitu vyote , Naye alifanya kila Taifa la wanadamu kutoka katika mmoja ,wakae juu ya uso wa Nchi yote , akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru ,tangu zamani na mipaka ya makazi yao, ili wamtafute Mungu ingawa ni kwa kupapasapapasa, wakamwone ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu, kwa maana ndani yake tunaishi tunakwenda , na kuwa na uhai wetu kama vile mmoja wenu, mtunga mashairi alaivyosema maana sisi sote tu wazao wake, Basi kwa kuwa sisi tu wazao wa Mungu haitupasi kudhani ya kuwa uungu ni mfano wa Dhahabu, au Fedha au jiwe, vitu vilivyochongwa kwa ustadi na akili ya mwanadamu, Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu.kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki kwa mtu Yule aliyemchagua naye amaewapa watu wote udhabiti wa Mambo haya kwa kumfufua katika wafu.

Simulizi: Paulo Akaanza kuwaambia juu ya uumbaji wa Mungu na mwenendo wake tangu zamani , Zamani Mungu alinyamazia Ujinga wa Mwanadamu na kujifanya hazioni, lakini sasa , Mungu anataka kila

mwanadamu afikilie toba, hivyo akaanza kuwajulisha habari za Yesu kwao, wengi waliskia na wakatubu na wengine walikaataan na wengine walidhihaki,

Maandiko: " Basi waliposikia habaria za ufufuo wa Wafu wengine walifanya Dhihaka, wengine wakasema tutakusikiliza tena katika habari hiyo ,Basi hivi Paulo akaondoka akawaacha, baadhi ya watu wakashikamana naye wakaamini katika hao waliokuwamo Dionisio Mwareopago, na Mwanamke mmoja jina lake Damari na watu wengine pamoja na hao.
Nukuu: Hali ikawa mbaya katika Berea ya Paulo na watu wengine, hivyo watu wa Berea walimtoa Paulo kutoka nje ya mji na kuanza safari yao kwenda Ethene, Athene ulikuwa mji dhaifu na mdogo ambao ulijaa sanamu na sheria zote zinazowakilisha kila aina ya Miungu walioiabudu , hivyo basi Athene ulikuwa katikati ya maeneo ya kuabudu miungu, kwa hiyo kulikuwa kuna sheria kali zinazomkasirisha Paulo na kushindwa na kuwaambia watu habari za Yesu,
Mahali pa kwanza Paulo kwenda kufundisha ulikuwa ni sinagogi (kama sehemu ya Mazoezi) Alikuwa akienda kila siku kuabudu, lakini wanaume wa Athene ikawa hawamwelewi Paulo, hivyo wakamchukua mlimani, (Areopagas) baada ya Mungu wao wa vita mara nyingine huitwa kilima wars, baada ya Mungu wa Roma wa vita, ambao watu waliitwa pamoja kuzungumza vitu tofauti tofauti pale, Paulo aliwaambia wao kuhusu habari za Injili ya Yesu kristo, katika mlima huo, Paulo aliona sanamu ambayo imeandikwa, mungu asiyejulikana, akainyoshea kidole, Paulo akasema ,kuna Mungu mmoja aliye mtakatifu asiyekuwa na uhitaji, Mungu Mwenye maarifa yote, Muumba wa kila kitu, bali wao walibaki kutumaini sanamu yao ambaye hawezi kufanya lolote, Akawaambia tena kuhusu sanamu na Dhambi, (Kwamba ilikuwa ni kosa) Inahitaji watu watubu Dhambi zao, kwani Mungu atahukumu kila mtu ambaye hajaamini wokovu wa Yesu kristo na kufufuka kwake. Baadhi yao waliomsikia Paulo walimcheka na kumdhihaki , wakaanza kufikiri kuhusu hilo , kwamba anachoongea Paulo ni kweli, nao wakaamini
Wajibu: Baadhi ya watu wanajua kwamba kuna Mungu, lakini hawakuelewa , kwamba alimtoa Mwana aliyekufa kwa ajili yetu , Mungu ametutuma sisi kuwaambia watu kuhusu Yesu, na kwamba mmujue yeye, Nukuu ya kwamba wakati Paulo hakuwa na muda wa maandalizi, ya kunena alikuwa akiongea na watu wa Athene , Alituma ujumbe kwenda kwa watu waliokuwa katika ngazi za juu, Mara nyingi alituma wakuu wenye fikra kubwa (Epimenides na Aratus) kutumia kile walichokijua , Kila mara inakuwa ni rahisi kushirikisha watu kile unachokijua na kuamini kutokana na kuelewa desturi zao.
Swali: Je wewe umejitosheleza na umejiandaa kushiriki ujumbe wa injili, popote pale ambapo utapata nafasi?, je umejaribu kuwaambia wengine kumuhusu Yesu kristo? Historia gani kutoka kwenye maandiko, ungetumia kufafanua ukweli wakati unapoenda kuongea na mtu mwingine kuhusu habari za Yesu kristo , utachukua Muda kutafiti kile kinachowahusu wao?

SIMULIZI YA 21: MUNGU AMTOKEA PAULO KWA MAONO USIKU KUMTIA MOYO
Matendo 18:6,9
Maandiko: Baada ya mambo hayo Paulo akatoka Athene akafika korinto " akatoa hoja zake katika sinagogi kila sabato , akajaribu kuwavuta wayahudi na wayunani,Hata sila na Timotheo walipotelemka kutoka makedonia ,Paulo akasongwa sana na lile Neno, akiwashuhudia wayahudi kwamba ni Yesu kristo, walipopingana naye na kumtukana Mungu , akakung'uta mavazi yake akawaambia , Damu yenu na iwe juu ya vichwa vyenu , mimi ni safi tangu sasa nitakwenda kwa watu wa mataifa.
Simulizi: Paulo na sila wakaenda korinto , mji uliojaa uovu na anasa za mwili , akawahubiria wayahudi kwamba Yesu ni masihi, lakini walikataliwa na kupingwa na kutukanwa , Paulo akakung'uta mavazi yake na kusema Damu yenu iko vichwani mwenu , mimi niko salama Hivyo basi mimi nitaenda kwa mataifa kuwaeleza na ndo maana leo mimi na wewe tuko hivi

Maandiko: Bwana akamwambia Paulo kwa maono usiku, usiogope bali nena wala usinyamaze kwa kuwa mimi ni pamoja nawe wala hapana mtu atakaye kushambulia , ili kukudhuru, kwa maana mimi nina watu wengi katika mji huu, akakaa huko muda wa mwaka mmoja na miezi sita akifundisha kati yao Neno la Mungu.

Simulizi : Baadhi ya wayahudi waliamini na kubatizwa vilivile na wakorinto wengi , hivyo Bwana akamtokea Paulo katika ndoto , wakati wa usiku, Paulo alikuwa amevunjika moyo na kuogopa kutokana na mwitikio wa wayahudi, katika mji, Bwana akamwambia Paulo usiogope bali endelea kunena na usinyamaze kimya kwa maana hakuna mtu atakayeweka mkono juu yako na kukudhuru wewe , kwa sababu nina watu wengi katika mji huu, Paulo akabaki kwa miezi 18akifundisha Neno la Mungu kwa watu.

Nukuu: shughuku ya huduma huko Ethene ,kundi kubwa (Paulo na wengine) wakaenda korinto mbali kilometer 74 na 46 kwa sababu ya eneo nzima kwamba korinto ilikuwa ni mji mkubwa, Paulo anasema Nimekuja kwenu katika udhaifu na uoga na katika kutetemeka, (katika hekima ya watu) Lakini Nguvu za Mungu 1Korinto 2:1-5Lakini alipokuwa akiwahubiria wayahudi , wao walibadilisha ukweli na walikuwa na uhasama juu yake (kuhusu yeye) ambayo hiyo ilimkasirisha Paulo , akawaambia Damu yenu iwe juu yenu , iwe juu ya vichwa vyenu mimi ni msafi , niko salama kwa maana mmefanya maamuzi mabaya na sasa mnataka kubeba matatizo, hivyo naenda kuhubiri kwa mataifa badala yenu , Paulo alikuwa amekata tamaa na kuvunjika moyo kwani alitamani wale watu wamwamini Yesu kristo, Paulo akatoka hekaluni na akaenda kwa mlango wa Nyumba ya karibu kwa mtaifa mtu aliyeitwa jina lake Yusto aliyekuwa akiishi Katika korinto kulikuwa na sanamu mbalimbali na madhabahu za sanamu ambao watu walitumia kufanya zinaa kama njia ya kuabudu na wakati walipozidi kuhubiri wakawakataa.

Baadhi ya watu walimwamini Yesu, akiwemo (cripus kayafa) kiongozi wa sinagogi , kuna baadhi ya wanaume na wanawake walimkubali Paulo,

(Akila prisca Timoteo na sila ) Paulo alipokelewa na akafurahi ,akashukuru, kwenda kwa Mataifa, wakati alipokuwa akitafakari jinsi Mungu alipomtokea kwenye maono na kumwambia usiogope kunena maana atakuwa pamoja naye na hakuna mtu atakayemdhuru , paulo akawa na ujasiri mkubwa wa kubaki korinto,kwa mwaka mmoja na nusu akifundisha Neno la Mungu,

Wajibu Wetu: Kuna muda mwingine unakuwa unakata tamaa , lakini lazima tukumbuke kwamba Roho Mtakatifu anaishi ndani yetu, wakati ndiye anayetupa uhakika, ,msaada ,ulinzi, na huduma, Tunakuwa watiifu kwa ajili yake , yeye huwa pamoja nasi tunapotangaza habari za Yesu kwa watu wote

Wakati wakiwa korinto, Paulo aliwaona watu wengi wakija kwa kristo hata viongozi wa sinagogi, (gaius wa Nyumba ya stephano)

KORINTHO 1:14-16 ,Stephano mwenyewe alikuwa mgeni wa nyumba ya gayo,(Gaius) hawa watu watatu walikua wa muhimu katika maisha ya Paulo , ukweli wa mahusiano yalisahaulika katika huduma , mahusiano yao yalitumika katika kuelezea ufalme wa Mungu,

Swali: wakati Paulo akihubiri katika korinto, wayahudi walimkataa na hata kuikana injili ya Yesu kristo, Ungefanyaje ikiwa injili ya Yesu kristo unapeleka kwa watu na watu wanakataa? Paulo aliendelea kwenda mlango mwingine akihubiri.

SIMULIZI YA 22: WANA SABA WA SKEWA WA KUHANI MKUU WAKIJARIBU KUTOA PEPO KWA NGUVU ZAO WENYEWE - Matendo 19:11-20

Maandiko: Mungu akafanya kwa mikono ya Paulo Miujiza kupita kawaida , hata wagonjwa wakaletewa leso na nguo zilizotoka mwilini mwake , magonjwa yao yakawaondokea ,pepo wachafu wakawatoka watu, Baadhi ya wayahudi wenye kutangatanga, nao ni wapunga pepo wakajaribu kulitaja jina la Bwana Yesu juu yao waliopagawa na pepo wachafu wakisema , Nawaapisha kwa Yesu Yule anayehubiriwa na Paulo.

Simulizi: Mungu akafanya Miujiza kupitia mkono wa Paulo , Na baadhi ya Wakuu wa wayahudi wakatii, (Na wana wa skewa nao walienda wakikemea mapepo) walijaribu kutaja jina La Yesu kwa wale wenye roho chafu wakisema “Nakuamuru kwa Jina la Yesu anayehubiriwa na Paulo,

Maandiko: Yule Pepo mchafu akawajibu akawaambia , Yesu namjua na Paulo namfahamu , Lakini ninyi ni akina nani? Na Yule mtu aliyepagawa na pepo mchafu akawarukia wawili akawaweza hata wakatoka mbio katika nyumba ile hali wa uchi na kujeruhiwa , Habari hii ikajulikana na wayahudi wote na wayunani ,waliokaa Efeso, hofu ikawaingia wote na Jina la Bwana Yesu likatukuzwa.

Simulizi: Yule roho chafu akawajibu , Yesu namjua na Paulo namtambua lakini nyie ni akina nani? Yule mwenye roho chafu akashindana nao wakakimbia nje ya mji wangali wa uchi na kujeruhiwa , hii ikaenea katika Efeso yote na hofu kubwa ikaja kwa watu na Jina la Yesu likatukuzwa .

Nukuu: Katika korinto Paulo alianza kuhubiri kwa wakuu wa sinagogi, na korinto wakuu wa Dini walipinga . wakawa na manung’uniko lakini Paulo alizidi kuhubiri kwa Bidii, Paulo akatoka kwenye hilo hekalu la masinagogi akaanza kuhubiri huko Tiro (19:9) alifundisha mchana siku sita kila siku kwa muda wa miaka miwili, na baada ya Muda Injili ikaanza kusikika katika eneo kubwa. Watu wengi wakaamini na wengi wakaponywa kupitia mkono wa Paulo , Lakini sisi katika ulimwengu wa sasa tunaona watu wengi mjini wanaotafuta nafasi ,nguvu, na afya kwa kuwekeza waliona umaarufu wa Paulo nao wakaamua kufanya hivyo kwa matakwa yao binafsi, Hawajaelewa nguvu iliyokuwa ikimsaidia Paulo kufanya hivyo na kutenda miujiza , walijaribu kuiga kile Paulo anafanya, hata wakaiga maneno ya Paulo kuhusu Yesu, lakini macho yao hayakuwa yakimtazama Yesu, bali umaarufu wa Paulo na kutaka faida kwa kufukuza mapepo, bali mapepo hawakuwatii wao, (kama walivyomtii Paulo)badala yake Yule mtu mwenye pepo wachafu kuwarukia na wote saba na kuwapiga nao wakakimbia nje ya mji wangali wa uchi .

Watu wa mji waliposikia kilichotokea kwa wale saba , wakashtushwa kwa sababu mwishoni walidhihirisha nguvu za Yesu, walizunguka kulitukuza jina La Yesu , Mungu alionyesha kuwa ana uwezo juu ya mapepo wabaya.

Wajibu wetu: Kunukuu kile kitu ambacho mtu mwingine na kuona alafu ukaiga na kufanya ni Hatari sana, tamaa ya kufanya hivyo ni kuonyesha hali ya kiburi , kwani kufanya vitu kama hivi ni kutaka umaarufu , yanaweza kukupelekea kuwa katika mashambulizi ya kiroho katika maisha yako binafsi.

Waumini wengi waliona kuchanganyikiwa na hali ya kipepo au vitabu waliokuwa navyo wakaamua kurudi majumbani mwao , na kukusanya vitu walivyonavyo na kuwaletea ,wakakandamizwa bila wao kutokujua wanafanya nini,

Maandiko : Na wengi wa wale walioamini wakaja wakaungama, wakidhihirisha matendo yao , na watu wengi katika wale waliotumia mambo ya uganga wakakusanya vitabu vyao ,wakavichoma moto mbele ya watu wote ,wakafanya hesabu ya thamani yake ,wakaona kwamba yapata fedha hamsini elfu, Hivyo ndivyo Neno la Bwana lilivyozidi na kushinda kwa Nguvu.

Simulizi: Watu wengi walioamini wakaacha upagani wao nao wakachanganywa na wakristo wengine , wakakusanya vile vitabu vya waganga na kuchoma, na idadi ya vitabu vilivyochomwa yapata 50,000 vipisi vya silva kwa namna hiyo Injili ya Yesu ikainuliwa.
Nukuu: Hofu ya wakristo wapya iliwafanya kutengenezwa maisha yao, na kujua kwamba kile walichokuwa wakifanya ni vifungo kwani ilikuwa ni kwa masilahi yao, na walikuwa wanakosea, lakini maandiko na mafundisho, iliwapa wao uelewa kuhusu Ufalme wa Mungu, kutokana na ukiri wao wenyewe na hivyo wakawa huru na katika vifungo, na hivyo wakiwa katika kurudi, waliwafundisha wapagani katika mji nao wakaanza kuwa na mtazamo mwingine , kwani uzoevu wa sanaa na uigizaji ulikuwa kawaida , walipokubali kuwa wakristo wakaleta vitabu vyao vya kiganga wakavichoma ,wakapokea mabadiliko kupitia nguvu ya Injili na hivyo wakawekwa huru kutoka kwa michanganyiko wao binafsi uliokufa.
Kazi :Mtazamo wa Ulimwengu ni mkubwa kuliko tunavyofikiri ,tatizo kubwa inaonekana katika kitabu cha Hukumu ambayo inaelezea Kila mtu alifanya linalopendeza machoni pake (Waamuzi 21:25) kufanya kitu ambacho ulimwengu unafurahia na kukubali ina hatari ya kukuangamiza kiroho katika maisha yako binafsi.
Swali: Je wewe una umaarufu gani Mbinguni? Je Mungu anakujua wewe? Je kuna tatizo gani ukiiga wengine ili uweze kujipatia?
Matumizi(Mafanikio ya Huduma) Mafanikio ya Huduma huko Efeso ilikuwa na matokeo makubwa mazuri , watu wengi wamefanyika waumini na wakaachana na maadili mabaya na sanamu , hasahasa wale waliokuwa wachawi, ambao walionekana wenye picha na taswira nzuri katika Madhabahu ya Diana , waumini wengi wakawa hawafanyi kujinufaisha kwa kazi zao ili kujipatia faida zao na familia zao, bali kipato chao kilizidi kushuka kwani walikuwa wakidanganywa na wale wachawi, Mchawi mmoja alianzisha namna yake.Alichagua Fedha kuliko njia njema za Mungu.
Wakati kanisa linazidi kueneza Injili ipasavyo , ndipo shetani naye alizidi kuinuka kinyume , Lakini kumbuka kwamba silaha zetu za vita si vya mwili, sii za mpango wa Mwanadamu awaye yeyote, Bali kwa Nguvu za Mungu anayeweza, kuharibu Ngome , sisi tunaharibu mapenzi ya shetani na kila kitu kilicho kinyume na Kristo na Elimu ya Mungu na kuteka kila Fikra ipate kumtii Kristo. Korinto 10:4-5.

SIMULIZI YA 23: PAULO AKIWA EFESO KWA MARA YA MWISHO

Matendo 20:16-25,28-32,36-38

Maandiko: Kwa sababu Paulo alikusudia kupita Efeso Merikebuni ,asije akakawia katika Asia , kwa maana alikuwa na haraka akitaka kuwahi Yerusalemu siku ya pentekoste kama ikiwezekana, Toka mileto Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa , walipofika pale akawaambia Ninyi wenyewe mnajua tangu siku ya kwanza , nilipokanyaga hapa Asia, jinsi nilipokuwa kwenu wakati wote nikimtumikia Bwana kwa unyenyekevu wote, na kwa Machozi, na majaribu yalionipata kwa hila za wayahudi, ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia Neno lolote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha waziwazi nyumba kwa nyumba, Nikawashuhudia wayahudi na wayunani, wamtubie Mungu na kumwamini Bwana wetu Yesu kristo ,Basi sasa angalieni nashika njia kwenda Yerusalemu , hali nimefungwa rohoni nisiyajue mambo yatakayonipata huko, Isipokuwa Roho Mtakatifu mji kwa mji hunishuhudia akisema ya kwamba vifungo na dhiki vyaningoja. (Matendo 20:16-23)

"Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa kitu cha dhamani kwangu kama kuumaliza mwendo wangu na huduma ile niliyopokea kwa Bwana Yesu kuishuhudia habari njema ya Neema ya Mungu , Na sasa tazameni mimi najua ya kuwa Ninyi nyote niliowahubiria Ufalme wa Mungu nikienda huku na huko hamtaniona uso tena.

Simulizi: Paulo alikuwa akiondoka Efeso kwenda mahali pengine pa huduma , naye akijua kwamba hatawaona tena ndugu na wapendwa wake , na akijua kwamba anapoenda miji ya Yerusalemu anajua kwamba ataenda kufungwa, anasema mimi nayahesabu maisha yangu si ya dhamani kwangu binafsi , hivyo yanipasa kufanya na kutimiliza huduma hii nilioipokea kutoka kwa Yesu kristo Bwana na kudhihirisha Injili ya Neema ya Mungu , Nimekuwa mwaminifu kwa wito wa Mungu na sio kwa zingine na wengine wasio wa kweli,

Maandiko : Jitunzeni Nafsi zenu na lile kundi lote , nalo ambalo Roho Mtakatifu amewaweka Ninyi kuwa waangalizi, ndani yake mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa Damu yake mwenyewe, Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu Mbwa mwitu wakali wataingia kwenu,wasilihurumie kundi , tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu ,wawavute hao wanafunzi wawaandame hao, kwa hiyo kesheni mkikumbuka ya kwamba miaka mitatu usiku na mchana sikuacha kumwonya kila mtu kwa machozi, Basi sasa nawaweka katika mikono ya Mungu na kwa Neno la Neema yake ,ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi, pamoja nao wote waliotakaswa. (Matendo 20:28-32)

Simulizi: (Paulo akasema kwao) kwa hiyo nijiongeze mwenyewe na waumini ambao Bwana amewapa :Paulo anasema, Mimi najua ya kuwa baada ya kuwaacha nyie kuna wengine watakuja kuharibu huduma hii na watainuka miongoni mwenu kwa elimu mbalimbali kwa kuwadanganya na mafundisho yao , Paulo anasema nimekaa nanyi na kuwafundisha miaka mitatu na kuhubiri ukweli , hivyo simameni kupitia kweli hii , na sasa nawaweka Ninyi kwa Bwana na kwa ujumbe wa Neema yake ,ambao itawajenga katika kweli.

Maandiko: Alipokwisha kunena haya, akapiga magoti akaomba, pamoja nao wote, wakalia sana wote, wakamwangukia Paulo shingoni, wakimbusubusu ,wakihuzunika zaidi kwa sababu ya lile Neno alilosema ya kwamba hawatamwona uso wake tena, wakamsindikiza hata merikebu, (Matendo 20:36-38)

Simulizi: Baada ya kusema hayo, Paulo alipiga magoti na kuomba pamoja nao wote, wakalia na kuhuzunika kwa ajili ya kuondoka kwake , wakambusu na kumkumbatia na hapo wakamsindikiza kwenda merikebuni.

Paulo alikaa Efeso pamoja nao kwa muda wa Miaka mitatu, muda huo aliwafundisha, kanisa likapandwa na kukua na likapanuka zaidi, wakachaguliwa viongozi watakaolisimamia kanisa kipindi Paulo hayupo, ilikuwa ni Muda wake wa kuendelea na umisheni alioitiwa, hivyo aliwahimiza wao kuzidi kufanya kazi ili wamalize vizuri, na waliweza kufanya hivyo kwani walipokea mafundisho mazuri ya huduma , kabla hajaondoka Paulo alipiga magoti na kuomba pamoja nao wote.

Kazi: Tuna jukumu la kuwaleta watu kwa Bwana , zote tunakuwa sehemu ya Familia yetu ya kiroho pamoja , sasa wanakuwa kaka na dada katika kristo. Hii ndio maana kuwa kwenda kanisani ni muhimu ili kushirikiana na kila mtu na kutiana moyo kila mmoja katika Bwana .

Swali: Unafikiri ni kwanini Paulo, aliona ni Muhimu kuongea na viongozi wa makanisa mara kwa mara? Je wewe ungewaruhusu watu ambao unawaongoza wawe karibu nawe katika huduma? Je umewahi kufikiri uhitaji wa kutiwa moyo katika huduma? Wewe unafikiri ni nani wa kukutia moyo?

SIMULIZI SEHEMU YA 24: HUDUMA YA PAULO KUKATALIWA YERUSALEMU.

Matendo 22:22-26

Maandiko: "Naye akaniambia enenda zako kwa kuwa mimi nitakutuma, uende mbali kwa watu wa mataifa, wakamsikiliza mpaka Neno lile, wakapaza sauti zao wakisema mwondoe huyu katika Nchi kwa maana hafai kuishi, walipokuwa wakipiga kelele, na kutupa mavazi yao na kurusharusha mavumbi juu,

Yule jemedari akaamuru aletwe ndani ya ngome, akisema aulizwe habari zake, kwa kupigwa mijeledi, ili ajue sababu hata wakampigia kelele namna hii, hata walipokwisha kumfunga kwa kamba , Paulo akamwambia Yule akida aliyesimama karibu,je Ni halali ninyi kumpiga mtu aliye mrumi naye hajahukumiwa bado,Yule akida aliposikia , akamwarifu, Yule jemedari akisema ,unataka kufanya nini? Kwa maana mtu huyu ni Mrumi"

Simulizi: Paulo aliporudi Yerusalemu, akaanza kupingwa na kushutumiwa na kundi kubwa la wayahudi , alipoanza kuhubiri na kushirikisha kama kawaida yake, kundi la watu wengi wakawa na hasira na kupiga kelele, wakisema, Wafutwe hawa watu Duniani , ilikuwa ni neema kwake yeye kuishi,

Hivyo mkuu akaamuru aletwe ndani na kuulizwa maswali, huku wakijiaanda kumchapa, Anasema Ni haramu kuwaaharibu warumi ambao hawakuhukumiwa? Akida aliendа haraka iwezekanavyo, kwa mkuu wake , na akaja kwa Paulo na kumuuliza kama yeye ni Mrumi, Paulo aliwajibu Ndio, siku iliyofuta wakamchukua yeye mbele ya Senadrin ili ahojiwe , Paulo akajieleza , hivyo kuhani mkuu aliamuru apigwe kofi la uso, na Paulo akamkemea, alipojua kwamba kumbe alikuwa ni kuhani mkuu ,Paulo akaomba radhi ,hapo akajua kwamba hapo kuna michanganyiko wa mafarisayo na masadukayo , Paulo akaanza kuzungumza kuhusu Ufufuo na wafu, kwa haraka upishano ulidumu baina ya masadukayo ambao hawaamini ufufuo, wa wafu na mafarisayo au masadukayo mkuu aliamuru jeshi lake kumwokoa paulo na kumpeleka akiwa salama ndani

Kazi: Mungu ana njia ya kuwapa watu Neno lake ,tunapokuwa watiifu hata kama kuna hatari.

Swali: Paulo alijua kwamba yuko hatarini alipokuwa akienda rumi , unafikiri ni kwanini aliweka matamanio katika moyo wake?

SIMULIZI SEHEMU YA 25: YESU AMWONGOZA PAULO SIKU ZOTE Matendo 23:11

Maandiko: "Usiku ule Bwana akasimama karibu naye ,akasema uwe na moyo mkuu kwa sababu kama ulivonishuhudia habari zangu Yerusalemu , imenipasa kunishuhudia vivyo hivyo Rumi nako" (Matendo 23:11)

Simulizi: Usiku uliofuata , Mungu alimtokea Paulo na kusema ,Uwe na moyo mkuu kwani kama ulivyonishuhudia Yerusalemu Vivyo hivyo na Rumi nako, Paulo alitakiwa kwenda kuhubiri na Rumi nako, Na sasa Mungu anampa uhakika, Paulo alichukizwa kwa sababu kulikuwa na watu, kama 40 walijifunga wenyewe kwa kiapo wakisema kwamba hawatakula na kunywa mpaka Paulo atakapokufa , Mtu mmoja mdogo ambae alikuwa kiongozi wa Eneo , alikimbia kwa Mkuu na kumwambia kwamba asimchukue Paulo mbele ya senakerebu siku iliyofuata , hivyo walipanga kumuuwa Paulo , hivyo mkuu akaamuru watu wake kumchukua Paulo kwa Felex Mfalme,

Felex akasema amri kutoka kwa kamanda mkuu ,na kumwambia Paulo asikilize kesi yake ,huku mshitaki wake akitokea Mbele yake , Ndipo akaamuru Paulo apelekwe kwa Herode Gerezani na kuhifadhiwa mpaka ufike muda wa kusikilizwa :

Nukuu: Baada ya hayo Kukatokea kutokuelewana na shutuma za senakerebu zilisikiwa , Ilibidi Paulo achukuliwe na kuhifadhiwa kwa ajili ya usalama wake kupelekwa kwa viongozi wa Warumi na siku ya pili, Yesu alimtia Moyo Paulo, akamwambia " Uwe na Moyo mkuu Paulo kwani umenishuhudia huko Yerusalemu , vivyo hivyo yakupasa unishuhudie na Rumi nako , sasa senkerebu alipokataa kumuhukumu Paulo ,wayahudi wakamchukia zaidi, pamoja kutokana na chuki waliapa kwamba hawatakula tena mpaka watakapomuuwa Paulo. Paulo alimtuma kwenda kwa maaskari ambao walimchukua yeye kwa ulinzi mkubwa kwenda kwenye eneo ambalo Felex Mfalme alikuwepo , Baada ya siku chache ,Festo alimchukua Paulo alionekana mbele yake kwa ombi la viongozi wa wayahudi ,wakifanya shutuma yao bila ya Ushuhuda ,Paulo anawaambia hana hatia katika hayo yote ya kudaiwa kwenda kwa kaisaria katika Rumi , hivyo festo akasema itakuwa hivyo,

Wajibu wetu : Sisi tunahitaji kuhubiri Habari Njema za Yesu , Mungu ametutuma kila mahali.Agizo kuu iliyokuwa imetolewa ni kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi wa Yesu , kama tulivyo wasafiri duniani wanafunzi wanatengenezwa

Swali : Unadhani kwa kusudi gani na kwanini Mungu amekuokoa? ,

Ngoja nikusaidie kwa jibu "Ili kwamba tuwe mashuhuda wake kwa watu"

Uko kazini kutengeneza wanafunzi kwa ajili ya nani?

SIMULIZI SEHEMU YA 26: PAULO MBELE YA MFALME AGRIPA

Maandiko: "Agripa akamwambia Festo, Mimi nami nilikuwa nikitaka kumsikia mtu huyu, Akasema utamsikia kesho" (Matendo 25:22)

Basi kwa kuwa nimeupata msaada utokao kwa Mungu, Nimesimama hata hivi leo nikiwashuhudia ,wadogo kwa wakubwa, ila sisemi Neno ila yale ambayo manabii, na Musa waliyasema kwamba yatakuwa ,Ya kwamba kristo hana Budi kuteswa na ya kwamba yeye kwanza kwa kufufuliwa katika wafu atatangaza habari za Nuru, kwa watu wake na watu wa mataifa, alipokuwa akijitenga hivi ,Festo akajitoa kwa sauti kuu, Paulo, una wazimu ,kusoma kwako kwingi kumekugeuza akili, lakini Paulo akasema sina wazimu ,Ee Festo Mtukufu bali Nanena maneno ya kweli na ya akili kamili, kwa maana mfalme anajua habari za Mambo haya, nami naweza kusema naye kwa ujasiri, kwa sababu najua sana ya kuwa hakuna Neno moja katika hayo asilolijua kwa maana jambo hilo halikutendeka pembeni, Mfalme Agripa je wawaamini manabii? Najua ya kuwa waamini, Agripa akamwambia Paulo kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa mkristo? Paulo akamjibu namwomba Mungu kwamba ikiwa kwa machache au ikiwa kwa mengi si wewe ila na hao wengine wote wanaonisikia leo wawe kama mimi isipokuwa vifungo hivi, Mfalme na liwali na Bernike na wale walioketi pamoja nao wakasimama, hata walipoondoka wakasemezana wakisema ,mtu huyu hatendi neno linalostahili kifo au kufungwa, Agripa akamwambia Festo ,Mtu huyo angeweza kufunguliwa kama asingalitaka Rufani kwa kaisari. (Matendo 26:22:32)

Simulizi: Baada ya kuonekana mbele ya kaisaria , Paulo alibaki kwa Felex na Festo kwa miaka miwili , wakati wa Paulo ukafika akaonekana mbele ya Mfalme akielezea na akaendelea kumshirikisha jinsi ilivyokuwa mpaka amekuwa mkristo na alipomaliza, Mfalme alimuuliza Swali zuri " Wewe unataka kunishawishi na mimi niwe mkristo? Paulo akamjibu napenda mbele za Mungu uwe kama nilivyo isipokuwa minyororo hizi, Mfalme na mke wake wakabaki kusema hakika huyu mtu ni mjinga anataka kufa , au kufungwa , Agripa akamwambia Festo huyu ndo Yule mtu ambaye alipaswa aachiwe, na hajasamehewa na kaisaria

Nukuu: sura ya 23 na 25, ya matendo ya mitume , Shutuma za Paulo na kufungwa kwa Felex na miaka miwili baadae Festo ambae alimwakilisha Felex kama msimamizi na mfalme agripa ambaye alikuwa ni Mfalme wa Yudea na Samaria , Aligundulika na warumi kwamba ni mwangalizi wa Yuda ,Alikuwa akishutumiwa kwa kutunga sheria (21;28) na kunajisi hekalu 24:6 na kupanga mipango kinyume na warumi ,alikuwa akishutumiwa kwa kufanya maamuzi 24:5-6 Paulo alishakutana na viongozi wa Baraza la wayahudi Felex na Festo ,kuhusu changamoto hizo na kwamba hawakupata chochote katika matendo yake. Na walikuwa wanamtakia kifo, lakini walimwacha aende Roma kwa sababu ya ombi lake la kwenda kumwona Kaesaria Agusto.

Wajibu : Mungu hutumia hata wakosaji, kwa utukufu wake kueneza ufalme wake , sasa Paulo akaenda Rumi ambapo Mungu alimtokea katika Ndoto, Mungu hufanya kazi kwa njia ya Miujiza ili Neno lake liweze kuhubiriwa , kama Paulo alipokuwa akienda Rumi kwa ajili ya Injili.

Swali: wakati wa miaka Mingi wa kifo chake , unafikiri Paulo alifanya nini alipokuwa pale ?

Nini kulikuwa cha muhimu kwa warumi na kwamba Mungu alitaka Paulo afanye pale?

Je umenukuu yaliyopo katika ushuhuda wa Paulo? Je unaweza ukaeleza kilicho muhimu zaidi?

Unafikiri ushuhuda wako unaweza kuwa ya muhimu kama wa Paulo? hivi na wewe unaweze kuhubiri Injili na ikawa na mwitikio?

SIMULIZI SEHEMU YA 27 PAULO APANDA MERIKEBU KWENDA RUMI Matendo 27:1-6

Maandiko: “Basi ilipoamriwa tuabiri,(Kuhubiri) hata italia wakamtia Paulo na kikosi kingine katika mikono ya akida mmoja jina lake Yulio wa kikosi cha Augusto, Tukapanda katika merikebu ya Adramitio, iliyokuwa tayari kusafiri mpaka pande za Pwani wa Asia ,tukatweka Aristarko Mmakedonia wa Thesalonike akiwa pamoja nasi ,siku ya pili tukawasili Sidoni,Yulio akamhifadhi sana Paulo ,akampa ruhusa kwenda kwa rafiki zake apate kutunzwa ,kutoka huko tukatweka tukasafiri chini ya kipro, ili kuukinga upepo maana upepo zilikuwa za Mbisho , Tulipopita bahari upande wa kilikia,na pamfilia tukafika mira mji wa Likia , Na huko Yule akida akakuta merikebu ya Iskanderia tayari kusafiri kwenda Italia ,Akatupandisha humo. (Matendo 27:1-6)

Simulizi: Baada ya hesabu ya Baraza la wayahudi , wakasimama mbele ya warumi viongozi Felix na festo na mfalme wa eneo lile Agusto na kudaiwa mashtaka kwa kiongozi kaesaria na akasafiri kwenda Rumi, huduma ya Paulo Yerusalemu ikafikia Mwisho na kutoka Yerusalemu akapanda merikebu kwenda Rumi

Ilikuwa ni wakati mbaya kusikia kuhusu Italy, kwani upepo ulikuwa mkali sana na hali ya hewa ilikuwa mbaya sana, akiwazuia wasifanye mambo mengi ya kimaendeleo , meli aliyokuwa akitumia Paulo ilijulikana kama cargo na ilikuwa haina Nguvu ya kukatisha mpaka Bahari ya Mediterania wakati wa Mwaka huo, kwa hiyo akida wa malipo, wa umisheni alichagua vyombo vingine kwa ajili ya Swala la usafiri

Safari ya Paulo kwenda Rumi ina maanisha uzoevu mkubwa , Paulo alibaki kuwa kimya akifanya maamuzi ambao ilimfanya awe mjasiri katika mchuano wa safari. ujasiri usiokuwa na mashaka unapatikana katika Bwana ,ahadi ambayo unazaa ushuhuda huko Rumi matendo 23:11

Maswali : Umefikiri ahadi kuu ya Mungu, inakufanya uwe makini wakati unaendelea na malengo yako?

Paulo alikuwa mtume wa Mungu katika Rumi ,kwa hiyo ilikuwa lazima aende rumi,

Nukuu: kwamba Paulo alipokea msaada kutoka kwa marafiki huko sidoni, pia nukuu kwamba alikuwa Julius akida

Mungu ni Mwaminifu katika kuwapatia watumishi wake wanaofanya kazi yake mahitaji yao

Nyongeza wa Muda wa kufundisha : Paulo hakuwa mwenyewe , alikuwa ameambatana na Luka na Mtu aliyeitwa Aristakos kwa wema , aristakos alikuwa pamoja na Paulo katika Efeso wakati walipokuwa katika kutoelewana kwa kutengeneza sanamu , Yeye alikuwa upande wa Paulo hata kaesaria na wakati Paulo alitumwa Rumi , akapata pia kibali ya kusafiri na Paulo , Mungu hufanya kazi kupitia uhusiano wetu .

SIMULIZI YA 28: PAULO AKIWA KWENYE MERIKEBU NA THORUBA KALI –Matendo 27:18-26

Maandiko : “ kwa maana tulikuwa tukipigwa sana na ile tufani siku ya pili yake ,wakaanza kuitupa shehena baharini, siku ya tatu wakatupa vyombo vya merikebu kwa mikono yao wenyewe, jua wala Nyota hazikuonekana kwa Muda wa siku nyingi, na tufani kuu ikatushika na tukakata tamaa ya kuokoka , na walipokuwa wamekaa wakati mwingi bila kula chakula , Paulo akasimama katikati yao akasema , wanaume imewapasa kunisikiliza mimi na kutong’oa Nanga huko krete na kupata madhara haya na hasara hii, sasa nawapeni shauri, iweni na moyo mkuu,kwa maana hapana hata Nafsi mmoja miongoni mwenu atakayepotea ila merikebu tu kwa maana usiku huu wa leo malaika wa Mungu ambae mimi ni wake ,na ndiye nimwabuduye alisimama karibu nami , Akaniambia Usiogope Paulo huna Budi kusimama mbele ya kaisari tena Mungu amekupa watu wote wanaosafiri pamoja nawe, Basi wanaume

changamkeni kwa maana Namwamini Mungu, ya kwamba yatakuwa vilevile kama nilivyoambiwa , Lakini hamna Budi kupwelewa katika kisiwa kimoja. (Matendo 27:18-26)

Simulizi: Dhoruba ikawa mbaya , wakaanza kurusha makasia yao ili meli iweze kuelea . Paulo akawaambia msisite huko krete lakini wao hawakusikiliza ,mwishowe meli ikawa inazidi kuyumba kwenye Dhoruba mkali, kwa siku kumi na nne wakipambana na Dhoruba na hawakula chakula , Panapo usiku Paulo alisikia Neno kutoka kwa Bwana kwamba hakuna atakayepoteza maisha labda Meli mpaka tufike Nchi kavu. Kadri ilivyozidi kukucha , Paulo akawaomba wachukue chakula ,wakachukua mikate wakamshukuru Mungu, nao wakala, na idadi yao ilipata watu 276 na kulipombambazuka waliona Nchi kavu , Na meli ilikuwa ikizunguka kwenye mchanga ikagota Nchi kavu , wote wakashukia Nchi kavu iliyoitwa Melita, watu wakawakaribisha wakawahudumia kwa utu wema.

Kazi: Paulo alikuwa akionywa na malaika wa Bwana kwamba nini ingetokea, na watatokaje nje, Yeye alikuwa na mapenzi ya kushirikisha hili katikati ya Dhoruba,

Swali: Mungu hutupa maonyo katika Maandiko, vilevile kupitia watu ambao tunashiriki Neno kwa pamoja . Je? wewe umelipokea Neno la Mungu kwa Imani?

SIMULIZI SEHEMU YA 29: MUNGU ATHIBITISHA USHUHUDA WA PAULO – Matendo 28:1-10

Maandiko: “ Tulipokwisha kuokoka ndipo tulipojua ya kuwa kisiwa kile chaitwa Melita, wenyeji wakatufanyia Fadhili sizizokuwa za kawaida, kwa maana waliwasha moto wakatukaribisha sote, kwa sababu ya mvua iliyonyeesha na kwa sababu ya baridi, Paulo alipokuwa amekusanya mzigo wa kuni na kuweka motoni, Nyoka akatoka kwa ajili ya ule moto ukamsongasonga mkononi, wenyeji walipomwona Yule nyoka akilewalewa mkononi wakaambiana, hakosi mtu huyu ni muuwaji ambae ijapokuwa ameokoka katika bahari, haki haimwachi kuishi , Lakini yeye akamtukisia motoni na asipate Madhara. ( Matendo 28:1-5)

Simulizi: Wakiwa katika nchi kavu Paulo aliwasadia kukusanya kuni kwa ajili ya moto, walipoanza kuweka kuni motoni ,Nyoka akatokea katika kichaka kwenye kuni ambazo ziliwekwa motoni,akajifunga kwenye mkono wa Paulo na akamtupa Mbali ,akaanguka , bali Paulo hakuumia wala hakuadhirika sehemu hiyo aliyong’atwa na Nyoka , Watu walitarajia kwamba Paulo anaweza akafa muda wowote , lakini baada ya kusubiri kwa Muda mrefu wakaona hakuna kilichotokea na wakaanza kufikiri na kusema kwamba Paulo alikuwa Mwana wa Mungu.

Maandiko: “Karibu na mahali pale palikuwa na mashamba ya mkuu wa kisiwa jina lake Publio , mtu huyo akatukaribisha kwa moyo wa urafiki, akatufanya wageni wake kwa muda wa siku tatu ,Ikawa baba yake Publio alikuwa hawezi homa na kuhara Damu, Paulo akaingia kwake akaomba akaweka Mikono juu yake na kumpoza ,Yalipokwisha kutendeka hayo, wengine waliokuwa na wagonjwa katika kisiwa wakaja wakapozwa , nao wakatuheshimu kwa heshima nyingi, Basi tulipoabiri wakatupakilia vitu vile tulivyokuwa na haja nayo” (Matendo 28:7-10)

Simulizi: Mtu mmoja alimwalika Paulo aende katika Nyumba yake, Baba yake mtu huyu alikuwa akiumwa sana, na Paulo akaja kwake na kumwombea na kumwekea mkono juu yake, akapona , watu wengi walipoona hayo , nao walioko Island wengi wao wakaleta wagonjwa wao kwa Paulo nao wakaponywa , Wakati huo ulikuwa muda wa Paulo kuweka muhuri

Kazi: Hatima ya Bwana kwa paulo , Safari ya mwisho huko Rumi , Mungu anatoa njia kwa watu wema pia na kuwasaidia , Tunapokuwa katika Mapenzi ya Mungu na kumtii yeye anakuwa pamoja nasi na kutusaidia

Swali: Mungu anatupatia yale tunayotaraji ?, 276 (Abria) waliokuwa wanatambaa , Na kuogelea chombo ilipozama (Matendo 27:37) Paulo kupitia Roho Mtakatifu ,aliwapa ujasiri na Mwelekeo ambao wameokoa maisha yao , Je una ujasiri kwa Mungu kwamba Mungu atamruhusu Roho Mtakatifu aje kukutumia wewe katika hali hiyo? Je Ushuhuda wako utatazamika kama Mtu ambae anaweza kuja katika hali ya Mtikisiko ?

SIMULIZI YA 30- PAULO ASHUHUDIA HUKO ROMA Matendo 28:16,23:30

Maandiko: "Tulipoingia Rumi Paulo alipewa Ruhusa , kukaa kwake mwenyewe pamoja askari Aliyemlinda". Wakiisha kuagana naye siku, wakamjia katika Nyumba Waliyokaa watu wengi sana,akawaeleza kwa Taratibu na kushuhudia, Mungu akiwaonya mambo yake Yesu ,kwa maneno ya sheria ya Musa ,na ya manabii, Tangu asubuhi hata jioni , wengine waliamini yale yaliyonenwa na wengine hawakuamini". (Matendo 28:23-24)

Simulizi: Paulo akiwa Ndani ya nyumba, hata ingawa kiongozi alikuwepo muda wote, na kwa miaka miwili kulikuwa na watu ambao walikuwa wakija kwake Mchana na Usiku , kama Alivyowafundisha wengi katika njia za Bwana, alihubiri na kufundisha kwa nguvu zote wakati wote bila woga

Na aliposhitakiwa huko Rumi, Paulo alibaki katika uwaminifu na wito wa Bwana na kulitangaza Jina la Yesu, kwa mataifa na mbele ya wafalme.

Kazi: Wakati sisi tunapokuwa katika hali ngumu, mara nyingi tunakata tamaa, tunapaswa kujua kwamba tuko chini ya Amri na utawala wa kimungu endapo sisi tukijua wenyewe kwamba ni msaada wa Mungu ndio utakayetuokoa ndipo nafasi yake huonekana katika maisha yetu tukionyesha utii , Upendo na ushirikiano wetu kwake, kama tunavyohubiri habari njema za Yesu kristo kwa njia ya ushuhuda wetu binafsi, Paulo akiwa ndani ya nyumba wakamfunga na Paulo akawaita viongozi wa wayahudi wakutane naye mara ya pili na kuwapa ushuhda wake , Paulo alieleza umisheni wake kwao.

Ilimgarimu siku nzima , na baadhi yao waliamini na baadhi hawakuamini, Neno la Paulo la mwisho kwao ,Lilikuwa limetoka kwa Nabii Isaya , Yeye alisema nenda kawaambie watu hawa wawe katika hali ya kusikiliza , lakini sio kupokea , wawe katika hali ya kutazama , lakini sio kuelewa , kuangalia mioyo ya watu hawa katika hisia , masikio yao yametiwa giza , macho yao ni vipofu, vinginevyo wanaweza kuona kwa macho yao na kusikia kwa masikio yao na kuelewa kwa mioyo yao na kurudi na kuweza kuponywa . (Isaya 6: 9-10)

Nb: Kwa hiyo Wokovu ulikuja kwa Mataifa haijalishi hawakuitikia.

Lengo letu limekaa sawa, Yerusalemu, Yudea, Samaria na hata miisho ya ulimwengu mpaka mataifa yote wasikie, Dhawabu yetu ni kubwa Mbinguni kutoka kwa Bwana wetu Yesu kristo na Baba yetu wa Mbinguni na wa milele yote

Je ni ajabu kusikia kwa Mwokozi wetu? Tukipongezwa , Vizuri sana, umefanya vema, vizuri mtumwa mwaminifu , Ingia katika katika Raha ya Bwana wako.